MUNGU AKIFAHAMIKA VIBAYA

Bwana akubariki. Niombeeni, usiku huu. Tumekuwa tu na manyunyu madogo na ya kutosha kubaridisha, ambayo twashukuru kwake, nami natumaini kuwa tutakuwa na mojawapo ya manyunyu ya kiroho upande wa ndani kutusaidia kidogo.

2 Naamini, Ndugu Neville, tutageuzia hilo kwako. Vipi basi? Mimi nikinena, napata kidogo. . .hiyo hewa nikiipata basi mimi . . .huu upara wangu hupisha hiyo na kufunga koo langu.

3 Sasa, nilitoa baadhi. . .kwa ajili ya maswali fulani usiku huu, na majibu ili tu. . .Kusudi letu kufanya hili ni kupata kilicho katika mioyo ya watu.

4 Nadhani hilo ni nzuri sana kwa mchungaji ku—kutoa hii, ndiposa apate kujua yale watu wanayowaza kama wataandika maswali yao na kupata kitu. Nami nadhani kila mmoja wetu ana wajibu wa kutoa nia zetu kwa wachungaji wetu na—na viongozi wetu wa kiroho, na mengineyo, na lo lote tuonalo, ili tuweze kufanya kila kitu kiende laini na vizuri, na kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

5 Kisha mimi. . .hata yapata nusu saa iliyopita nilikuwa tu na mawili au matatu ambayo. . .Billy aliyachukua baada ya ibada asubuhi hii akaniletea. Halafu nikaja na kuyachuguza kwenye Maandiko, nilidhani ningenena kidogo usiku huu, kwa kuwa nilikuwa nimelitaja, na kwa kuwa niko hapa. Ndiposa yeye aliniita dakika chache zilizopita, kasema, "Hebu ngoja, ninayo machache sasa."

6 Kwa hivyo nitajaribu kuingia moja kwa moja kwenye haya na kuyajibu vema kadiri nijuavyo. Halafu nikimaliza kwa wakati, nina somo ambalo ningetaka ku—kunena juu yake kwa karibu dakika ishirini au thelathini hivi, somo fupi tu.

7 Ndiposa, kumbukeni, Bwana akipenda, Jumapili ijayo asubuhi nataka nifanye kadiri niwezavyo, kwa neema ya Mungu, kueleza yale Majuma Sabini ya Danieli. Kama nilivyosema asubuhi hii, ni Andiko kuu. Na sio sana kuongea juu yake, bali kuyaweka mahali pake, kuyafanya yalingane na sehemu nyingine zote za Biblia nyingine yote.

8 Nasi tumeanzia toka Ufunuo 1, tukafikia kwenye sura ya 6. Na, hakika, tunaingia sasa kwenye zile Muhuri saba za mwisho. Na Muhuri zile zitaanzia sura ya 6, sehemu ya mwisho ya sura ya 6, hata sura ya 19, pamoja. Kwa hivyo itachukua muda mrefu. Sasa, ningechukua, tuseme, siku saba, na kuzipitia zile Muhuri Saba, nikizifunua. Lakini ukifanya hivyo, watu watakosa shehemu kubwa nyuma *hapa* inayojaza hili. Na kama

hawajafunzwa vilivyo, huenda isiwe nzuri. Lakini za kwanza tatu au nne ni matukio tu ambayo twaweza kuongea juu yake, yakija tu yamefuatana; lakini zinazofuata; basi yakupasa urudi nyuma katika Danieli tena, urudi tena katika Mwanzo, urudi katika Ufunuo, urudi katika Injili, na uzifungamanishe zote ndani mle, kwa sababu ni kufuatilia Israeli, Mungu akishughulikia Israeli. Maana Kanisa lipaapo juu, huo ndio mwisho wa Kanisa hata litakapokuja pamoja na Bwana Wake kama Bibi-arusi na Bwana arusi katika sura ya 19; katika wakati huu anashughulikia Israeli. Na kupata yale Majuma Sabini ya Danieli sasa, kunatayarisha kule kufunguliwa kunakokuja, Muhuri wa Kwanza.

9 Ndipo nilidhani, Bwana akipenda, mimi. . .Jumapili ijayo ningenena kuhusu hayo. Nisipomaliza Jumapili asubuhi, basi nitajaribu tena Jumapili usiku. Na hilo lingefungua njia basi, kama Bwana atatuongoza, haitatupasa kukoma katika sehemu hiyo, tungeenda moja kwa moja katika zile Muhuri Saba na kuendelea nazo kwa kadiri tutakavyoona Bwana akiongoza.

10 Sasa, usiku huu tuna maswali kadha, na yote ni yenye busara, maswali yanayofaa. Kulikuwa na moja ndani humu ambalo ningetaka kuzungumzia kwanza, kwa dakika chache. Ilikuwa mtu fulani aliyeuliza. . .Si swali, ni mtu fulani aliyeniuliza tu:

Funguo zangu ziko wapi? Tafadhali niambie.

11 Wao—wao walikuwa wamezipoteza adhuhuri ya leo. Sasa, nawaambieni, majuma machache yaliyopita, yapata siku chache zilizopita nilikuwa hapa Maskanini. . .Nilikuwa nikiomba na kumngoja Bwana na kutafuta mahali ambapo vitu hivyo vilikuwa kwa ajili ya watu. Nimepata motokaa za watu. Bwana angeniambia mahali ambapo watu wange. . .

12 Ndugu Welch Evans alikuja hapa na akapoteza motokaa yake, mtu fulani aliiiba huko Louisville. Yeye na Ndugu Fred Sothmann na baadhi ya ndugu. . .Ndugu Tom Simpson, naamini, alikuwepo siku hiyo. Au sivyo, Ndugu Tom? Nao walikuja hata nyumbani, na pale alikuwa Ndugu Evans bila motokaa, bila nguo, kila kitu alichokuwa nacho kilikuwa katika motokaa hiyo. Nao waliipeleka kwa Miller na mtu fulani akaichukua.

13 Vema, tuna njama za wizi ama ujambazi unaoendelea hivi sasa kule Louisville, ambapo wanayaiba magari haya na wangeyapeleka kule Bowling Green au mahali kama hapo na kuyapaka rangi tena. Na katika Kentucky haikupasi uwe na hati ya kuthibitisha kwa gari lako, nao waweza kugeuza magari hayo katika dakika chache na wayauze kwa njia yo yote waliyotaka.

14 Vema, Ndugu Evans na gari lake ndogo na vyote alivyokuwa navyo ndani humo, basi Bwana akanipa jibu. Na kabla hata hawajafika nyumbani, gari lile lilikuwa limesimama pale nje

likiwa na petroli nusu, ambapo Yeye aliwageuza njiani kuelekea Bowling Green, na kuwarudisha na kuweka gari lile nyuma kule na kila kitu ndani yake, hakuna hata kimoja kilichokosekana, ila tu petroli iliyotumika.

15 Mara nyingi watu wamesema mambo *fulani,* na wangeuliza, nami ningeenda mbele za Bwana na kungoja maono hayo, naam, nikingoja hata hayo yaje. Lakini natambua kuwa hilo limeleta kikwazo kikubwa mbele ya watu. Hakika, watu wa Amerika hawako tayari kwa huduma kama hiyo, makanisa. Hiyo ni kweli. I—imepita wakati wao. Mwaona? Na inasababisha kila kutu, wengine wanakuita "shetani," wengine wanakuita "mnenaji na mizimu," wengine hukuita "mwana wa "Mungu," "mungu," na kila kitu. Waona? Kwa hivyo nilimuahidi tu Bwana kuwa nitaiachilia iondoke na ningojee tu ndiposa nitumie huduma hiyo kule Afrika au kwa mahojiano ya kibinafsi ninapokuwa nayo hapa.

16 Sasa tuko hapa kwa mahojiano ya kibinafsi, ambayo bado huendelea juu ya mambo kama hayo. Lakini . . . Na njia ya kuyapata si kuja kanisani, unaenda kwa katibu wetu, mwanangu, Billy Paul, naye atakupa . . . kijikaratasi kidogo akikwambia itakuwa lini na mengineyo. Na lo lote kama hilo, hayo ni kwa mahojiano ya kibinafsi, hapa au kule nje, yaweza tu kuja hivyo. Kuna u—ubao ulioandikwa hayo, au kitabu, au karatasi kwenye ubao wa matangazo pale, jinsi ya kufanya hayo. Lakini kuja tu hapa jukwaani . . .

17 Sasa, tuna karama kanisani. Tuna Ndugu Neville hapa ambaye amepokea karama ya unabii. Ndugu Higginbotham anayeketi hapa, aliye na karama ya kunena kwa lugha na kufasiri lugha. Ningewapa ninyi wosia . . . Nitaomba ya kwamba Mungu atakupa funguo zako, lakini nita—nitakushauri kuwa labda kama Roho Mtakatifu angenena usiku huu, labda, kupitia Ndugu Neville au Ndugu Higginbotham, au baadhi ya karama hizi kanisani, kwamba tuna maswali kadha juu yake katika dakika chache, kuwa labda wangefanya hivyo.

18 Lakini, kwangu mwenyewe, nimemuahidia Mungu, hapana tena humu Amerika katika mikutano ya hadhara, waona, kwa sababu lilisababisha mimi kuacha kuhubiri. Basi wengine watakufanya kuwa "she—shetani," wengine watakufanya "Mungu." Na kwa hivyo mwaona, hawako tayari Kwake. Na kwa hivyo Mungu hawezi kufanya hilo, nami nina hakika mtu yule aliyeuliza atafahamu. Sasa, labda Roho Mtakatifu bado usiku huu . . . Endelea tu kuomba. Nitaomba kuwa Roho Mtakatifu atakuonyesha kiliko kifurushi chako unachokingoja. Naomba kuwa utakipata, nami naamini utakipata. Waona?

19 Na . . . lakini sasa . . . Ndiposa, sasa, Billy Paul, mtu fulani akiwa na jambo kama hilo, na wamwite, yeye angemrejeza

kanisani, nami hujaribu kukabiliana na hali za hatari ninapokuwa nyumbani.

20 Sasa, hebu sisi, sasa kabla hatujayaendea maswali haya... Kwanza, nataka kusema kuwa swali lo lote lisilolingana na imani yako au...katika Biblia, halilingani na Neno, basi haikupasi kulipokea. Basi ili niende kule chini na labda nipate somo pia usiku huu, ningependa kuendelea na kuyajibu na yale ninayodhani kuwa—kuwa yana majibu ya Kimaandiko, vema, nitayajibu, kila kitu niwezacho. Lakini niliyapata tu dakika chache zilizopita, yote ila matatu, wala hayo matatu hayana... Mambo madogo madogo kuhusu mtu fulani aliyeota ndoto au mengineyo, wakitaka kujua kama wangesimulia, au mengine kama hayo, mwaona.

Kwa hivyo hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa tunapokaribia rehema Zake.

21 Bwana, sisi tu watu Wako tulioitwa kwa Jina Lako. Nasi tuna furaha sana usiku huu kujua kuwa sisi tuna Baba wa Mbinguni anayetulinda na kutushughulikia, na hutupenda kama watoto Wake Wapendwa. Na kwa hivyo nina furaha tele, Bwana, ya kuwa nimehesabiwa pamoja na watu hawa, kuwa ndugu yao, nao ni ndugu na dada zangu. Nina shukrani sana.

22 Kunaye mmoja, Bwana, ambaye amepoteza funguo. Wewe wajua pale zilipo. Naomba kuwa Wewe utafunua na uzilete moja kwa moja funguo hizo. Ni kitu cha thamani kwao, ni za gari lao. Nami naomba, Baba, kuwa Wewe utawajalia ombi hili watu hao.

23 Sasa naomba kuwa Wewe utambariki mchungaji wetu, Ndugu yetu mpendwa Neville. Tuna furaha sana kuona Wewe ukifanya kazi kati yetu katika hizi karama kuu za kiroho kanisani mwetu, sehemu ya mwili wa Kristo inayoabudia pembeni humu mwa Nane na Penn. Tuna furaha sana kuhesabiwa pamoja na kundi hilo la watu, na kujua kuwa Mungu hufunua siri kwa watu Wake. Naomba kuwa utambariki Ndugu Neville, mchungaji wetu, na Ndugu Higginbotham, Ndugu Funk, Ndugu Junior Jackson, na dada zetu wanaonena kwa lugha na kufasiri. Twaomba, Baba, kuwa Wewe utaendelea kujidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa hizi karama kuu, kanisa letu lipate kujulikana kama kanisa la Kiroho, ambamo watu waliochoka waweza kuja na kuketi katika Uwepo wa Mwenyezi Mungu na kujua Yeye hunena na kufunua siri za moyo.

24 Pia Baba, naomba kuwa utatubariki sisi usiku huu katika kujibu maswali haya. Baadhi yao, Bwana, ni rahisi, na mengine yao ni magumu. Kwa kila mmoja aliyeuliza swali, ni swali gumu. Ni kitu kilicho mioyoni mwao, wanataka kitatuliwe. Na, Baba, sote hatutoshi kwa wajibu hizi, bali tunajua Wewe ni unatosha bila shaka. Kwa hivyo twaomba kuwa Wewe utafasiri maswali haya kwetu, ili tuweze kuwapa watu majibu sahihi, wapate kusaidika na kanisa likatukuzwe, Jina la Mungu likaheshimiwe.

25 Sasa, Baba, ikiwa ni mapenzi Yako, naomba kuwa utatushughulikia sisi juma hili na utanisaidia mimi ninapochunguza kwa makini hayo Majuma Sabini ya Danieli, niweze Jumapili ijayo, kama ni mapenzi Yako, kuwafunulia Maandiko watu hao. Mungu, tujalie, kusudi nafsi zao ziweze kuburudishwa. Wafundishe hao, Bwana, wanaotafuta mambo yenye kilindi. Waokoe wale wamepotea. Waponye walio wagonjwa. Sisi sote tunakungoja Wewe, Baba. Katika Jina la Yesu. Amina.

26 Sasa swali hili la kwanza si swali hasa, ni kitu kidogo tu kwa ajili ya . . . Aisee, nasimama karibu sana na hii? Je, sauti inasikika vibaya, nyuma kule? Kama ndivyo, inua mkono wako.

132. Ndugu Bill, tafadhali sema neno kuhusu watoto na watu wazima wanaofanya kelele nyingi asubu- . . . wakitembea hapa na pale wakati wa ibada. Maskani haya yanahitaji mafundisho kuhusu kicho.

27 Amina! Watoto, hamjui jinsi ya kutii katika nyumba ya Mungu? Je, hamjui hapa ni mahali patakatifu pa Mungu? Mungu yumo katika hekalu Lake takatifu, na kila mtu anyamaze. Ni mahali pa Mungu ambapo watu wanakuja, wakitafakari, wakijaribu kupata wokovu kwa nafsi zao; wakijaribu kutafuta shida za maisha ya watu, wakijaribu kumsaidia mtu fulani. Yote iwapasayo kufanya ni kuwa na kicho, kunyamaza. Kunywa maji kabla kanisa halijaanza, najua watoto hawana budi kunywa. Mama walio na hao watoto wachanga, kama mngeketi karibu kule nyuma, muwanyamazishe mwezavyo. Na hampaswi hata kunong'onezana kamwe, kunong'onezana hata kidogo. Sisi sote tuna hatia. Lakini Biblia hiyo inaposomwa na huyo mhudumu anaingia mimbarani, yatupasa kunyamaza, tukimngoja Bwana. Sasa, tafadhalini mjaribu kufanya hivyo.

28 Najua, ninyi watoto, hamna budi kuvinginyika kidogo. Hivyo, mkifanya hivyo, fanyeni tu—iweni wazuri sana. Pia, kumbukeni, mama hataki ninyi mfanye hivyo, na baba hawataki mfanye hivyo, na kwa hivyo . . .

29 Nami najua, nina watoto wachanga, pia, wanaovinginyika hapa na pale, na Joseph. Na Meda husema, "Sisikii cho chote ibadani, kwa kujaribu kumnyamazisha Joe." Vema, yeye anajaribu kufanya hilo ili mtu mwingine aweze kupata kitu katika ibada. Mwaona?

30 Nasi kila mara twataka kustahiana, kuheshimiana sisi kwa sisi. Na, zaidi ya mambo yote, mheshimuni Mungu na muiheshimu nyumba Yake.

Sasa, hili swali linalofuata ni:

133. Watoto wawili, mmoja mwenye umri wa miaka toka sita hadi minane, walikuwa hapa madhabahuni asubuhi hii. Unashauri inawapasa kubatizwa mapema jinsi gani?

31 Mara tu mwezapo. "Tubuni mara moja mkabatizwe," hiyo ni, katika Jina Lake Yesu Kristo. Sasa, hilo ni swali namba moja. Ningeshauri hivyo. Lakini twaona katika Maandiko . . .

32 Mnasema, "Je, hilo ni la Kimaandiko?"

33 Petro alipohubiri kwenye ile Siku ya Pentekoste, watu elfu tatu waliokoka na kubatizwa wakati ule ule. "Nao waliomwamini Bwana wakabatizwa." Kwa hivyo mara tu unapomwamini Bwana na kumkubali Yeye kama Mwokozi Wako, enda moja kwa moja majini ukafanye maungamo yako kuanzia papo hapo; vijana kwa wazee, haidhuru yu nani.

34 Mnasema, "Vema, huenda watoto hawa ni wadogo sana."

35 Yesu alisema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa Ufalme wa Mungu ni wao." Singethubutu kumzuia mtoto atakayekuja madhabahuni au kubatizwa, kwa umri wo wote, sijali wana umri gani.

Sasa swali la pili:

134. Mhudumu rafiki yetu hubatiza katika jina la "Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu." Je, tungehukumiwa kwa kutokumwambia kosa lake?

36 Naamini, kama Mkristo, una wajibu, na kama yeye yu rafiki wenu . . . Si kuzusha ubishi naye; ukifanya hivyo, basi wewe hauko sawa, roho ya—yako haiko sawa. Lakini kama unampenda ndugu huyo, na hapana shaka unampenda, kwa sababu ulisema, "Rafiki mhudumu." Basi . . . Hakuna jina limeandikwa kwenye vijikaratasi hivi, sijui vilitoka kwa nani, haya maswali.

37 Sasa, ningekushauri, ye yote yule, kama mhudumu huyu hubatiza hivi, nawe unamtembelea nyumbani kwake na mengineyo, ninge—ningetaja tu swali hili wakati mwingine. Na hilo huenda likakupa . . . Ongeeni tu hata mtakapolifikia, endelea tu kuongea kulihusu, kulizunguka; na mwache Bwana alifunue, ndiposa ni Bwana anayekwambia ulifanye. Waona? Ngoja tu hata Bwana akufunulie swali lile. Ndipo mwambie, useme, "Ndugu, nashangaa, kama Maandiko ya Mathayo 28:19 na Matendo 2:38, na kuendelea, je, kuna kuhitilafiana pale? Waweza kueleza mbona mmoja alisema hapa, 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,' na mwingine akasema, 'Jina la Yesu Kristo'."

38 Sasa—sasa, usijaribu . . . Kama wewe si mwanafunzi halisi, na hujui unalonena, heri liache. Waona? Waweza tu kumwambia, useme, "Vema, ningependa ungelikuja . . . " Kama yeye aonekana mwenye moyo mweupe, sema, "Nashangaa kama ungekutana na mchungaji wetu au mtu fulani na mlijadili?"

39 Nawaambieni, ni jambo lenye kilindi. Waona? Usijichukulie mwenyewe, kwa sababu huenda ukajitatanisha. Na kama una . . . Sasa, kama unajua yale unayonena, na una dhati na unajua Maandiko, vema. Lakini usimkasirishe, kwa lo lote

unalofanya, usimuudhi. Waona. Usimchukize, mwambie tu hivyo . . .

40 Naam, hakika, yeye amekosea. Hiyo ni kweli. Mtu huyo amekosea anapobatiza hivyo. Na mtu ye yote abatizaye kwa jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" amekosea kimaandiko. Hiyo ni kweli.

Swali namba tatu:

135. Katika taarifa ya imani, wao husema, "Twaamini Mungu mmoja, Wa milele aliye katika nafsi tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Mathayo 28:19, 18 na 19; Wakorintho . . . wa Kwanza 13:14. Si hizi zapaswa kuwa ni afisi tatu badala ya nafsi tatu?

41 Uko sahihi! Hamna nafsi *tatu* katika Uungu. Na haiwezekani kuwepo nafsi pasipo kuwepo mtu, hapana budi kuwepo mtu kusudi nafsi iwepo. Hakuna Miungu mitatu. Kunaye Mungu mmoja tu, na Mungu huyo ni Yesu Kristo. Mungu ni Roho aliyekaa katika Yesu Kristo, na yuaishi katika Kanisa Lake (wewe na mimi) leo, akijigawanya Mwenyewe kwetu katika umbo la Roho Mtakatifu, ambaye ni Mwenyezi Mungu, Mwenyewe akiishi ndani yako.

42 Sasa, uko sahihi, ni "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," ni afisi tatu za Mungu yule yule. Lakini, si Miungu mitatu, hilo kulingana na Maandiko ni kosa.

136. Je, Mkristo aweza kuenda Mbinguni ikiwa yeye halipi fungu la kumi?

43 Sasa, hilo ni moja ambalo singaliweza kujibu, kimaandiko.

44 Sasa, hili "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," kama mhudumu huyo yuna moyo mweupe, hebu—hebu tujue, mwaona, tungefurahia . . . Ndugu Neville pamoja nami, au Ndugu Beeler, au Ndugu Collins, au ye yote wa wahudumu hawa hapa ambao wameagizwa kwa huduma hii, na wengineo, aweza—aweza kufanya hivyo.

Sasa, lakini basi: **Je, Mkristo haendi Mbinguni kwa sababu wao hawalipi fungu la kumi?**

45 Si—singesema "ndio" au "la" kwa hilo. Lakini naamini kuwa kila Mkristo apaswa kulipa fungu la kumi kwa sababu ni maagizo ya Bwana. "Na heri ni . . . wale watendao maagizo Yake yote, ili wawe na haki ya kuingia katika Uzima, ule Mti wa Uzima." Basi, naamini kuwa fungu la kumi ni muhimu kwa ujuzi wa Mkristo. Kwa maana nitafikia hilo katika swali lingine katika dakika chache, najua kunalo lingine ndani humu linalohusiana na hilo.

137. Ndugu Branham, nimeokoka na nimebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, lakini nitamwepukaje pepo mkaidi ambaye yaonekana siwezi kujitoa kwake?

46 Vema, ndugu yangu au dada Mkristo, ye yote yule, sasa, wakati mwingi unapokutana na watu walio na pepo wakaidi, kwa kawaida ni kinyongo kinachosababisha hili, huenda ikawa wameirithi toka kwa mama, baba, mjomba, shangazi, au nyanya, babu mtu kama huyo. Na ukichunguza kote maishani mwako, utaona . . . Sasa, nimeipata kwa ujuzi, chini ya upambanuzi; kwa sababu ni mekutana na hali hizo jukwaani, maelfu ya watu waliokuwa na pepo huyo. Na jambo la kwaza wajua nitafuatilia pepo huyo kule nyuma kwa upambanuzi na kuona kuwa kulikuwa na babu, kulikuwa na nyanya, kulikuwa na mtu mwingine nyuma kule, na unarithi hiyo kwa maumbile.

47 Kaidi—ukaidi si wa Mungu. Na sasa njia pekee ya kuepuka hayo ni kwamba yakupasa uwe na imani ukaushinde huo, ya kwamba, wewe u Mkristo. Wewe u mwana au binti wa Mungu, ye yote uliye, na hutaweza kamwe kusimama na kuukemea na kuukemea na kuukemea. Ni kama tu kumchezea nyoka mkali mwenye sumu, yeye amekaa pale tayari kukuuma. Kama hutamjali na umuache, yeye hawezi kukudhuru. Waona?

48 Kwa hivyo unapojisikia una pepo kaidi, weka kitu kile madhabahuni, na umwamini Mungu kuwa kitu kile kimekufa na hutakuwa nacho kamwe, na uendelee na hata usikijali tena, na kitu hicho kitakuacha. *Mpinge* Shetani naye atakukimbia, hayo ni, "Ondoka upesi." Kwa hivyo hilo lingekuwa shauri langu jinsi ya kumshinda. Tunamshinda Shetani kwa imani. Hicho ndicho tushindiacho maovu yote, ni kwa imani.

138. Mbona wewe hubatiza kwa Jina la Yesu Kristo badala ya "Baba, Mwana na Roho Mtakatifu?"

49 Vema, hakuna kitu kama jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Hiyo ndiyo sababu. Hakuna ye yote katika Biblia aliyepata kubatizwa katika Jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Kila mtu katika Biblia, au miaka mia tatu upande huu wa Biblia, alibatizwa kwa Jina la Yesu Kristo. Hakuna mtume hata mmoja, hakuna hata Mkristo mmoja, hakuna wakati hata mmoja ambapo "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" iliwahi kutumiwa kwa ubatizo hata kanisa Katoliki lilipoundwa kwenye Baraza la Nikea, miaka mia tatu na sita baada ya kifo cha mtume wa mwisho.

50 Hakuna kitu kama jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Baba si jina, Mwana si jina, Roho Mtakatifu si jina. Ni vyeo vitatu, vyeo vitatu vya afisi ya Jina moja: Yesu Kristo. Kwa hivyo basi hamna kitu kama jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Na si . . . Hamna jina kwake, kwa hivyo nabatiza kwa Jina la Yesu Kristo ambalo ni Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ni dhahiri?

139. Watu wengine husema kuwa "Kristo alikuwa Kuzimuni kabla hajafufuka." Je, hili . . . Je, kuna Andiko kwa hili?

51 Naam, hapa kuna swali la Kimaandiko ningependa kukujibu toka kwa Maandiko, kwa sababu wameuliza, “Iko katika Maandiko?”

52 Ningependa kama mngefungua pamoja nami I Petro 3:18 na 20, ninyi mnaotaka kulisikia, ikiwa uliuliza swali lile au la, ili msilazimike kuchukua neno la mtu mwingine. Mwaweza kulisoma na kuona kama ni kweli au la. Sisi kila mara tunataka kukaa na Kweli, na ambapo Biblia hulinena. Na mtu huyu mpendwa, ye yote yule, ameuliza akitaka kujua kwa kurejea katika Biblia kama hili ni kweli au la.

53 Sasa, twapata hili katika . . . Kama nimelipata. Biblia hii zee karibu imepasuka, hapa, ambayo ni—nimekuwa nayo kwa miaka kadha. Kama naweza kuona iwapo nimelipata hapa, nadhani labda . . . Hebu sekunde moja, ndugu, kama nina—nina—hakika kuwa ndipo . . . Hebu tuone, inafuata Timotheo, Tito, na Waebrania. Ndiyo hii, hapa, naam, nimeipata. Asante. I Petro 3, sura ya 3 ya I Petro. Sura ya 3, basi hebu tuanzie ki—kifungu cha 18:

> *Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali Roho yake akahuishwa,* (akahuishwa kwa Roho).
>
> *Ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri;*
>
> *Watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji.*

54 Sasa fungua Matendo 2, Matendo 2, nasi tutachukua ki—kifungu cha 30. Katika Matendo 2, na huyu ni Mtume Petro pia akinena. Matendo, sura ya 2, na ki—kifungu cha 30 nimekiandika hapa:

> *Basi . . . kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha Kristo katika kiti chake cha enzi;*
>
> *Yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili* Wake haukuona uharibifu (Mwili wa Kristo).

55 Nafsi Yake iliingia kuzimuni na kuwahubiri roho, au nafsi ambazo hazikutubu katika ule uvumilivu katika siku za Nuhu. Nafsi Yake iliingia kuzimuni na Yeye akawahubiri wale roho, na akafufuka siku ya tatu. Hilo ni Maandiko, Kweli.

140. Sasa, wale wanawali watano walipotea?

56 Nadhani kwamba wanauliza swali, "wale wanawali watano," wale wenye busara watano na wapumbavu watano. Sasa, kama ulikuwa pamoja nasi katika yale mafundisho ya mwisho katika Ufunuo, uliona pale kuwa hao wanawali, wale—wale wanawali watano wapumbavu hawakupotea; lakini hawakuruhusiwa kuingia katika ile Karamu ya Arusi, lakini walipata mateso na wakauawa, na kufufuliwa tena katika ufufuo wa watu wote katika siku ya mwisho. Hao ndio wale watu ambapo Yeye aliwabagua kondoo na mbuzi, waona, wao walisimama Hukumuni.

57 Mnasema, "Vema, Ndugu Branham, sisi hatutasimama, Kanisa?" La, bwana! Hatusimami Hukumuni.

58 Sisi sasa tunasimama katika hukumu, Mungu aliweka dhambi zetu juu ya Kristo, na sisi... "Yeye alisikiaye Neno Langu," Yohana Mt. 5:24 "na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala haingii Hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hakuna tena hukumu kwa Kanisa. Linanyakuliwa, na linarudi tena kuwahukumu watu ambao hawakumpokea Roho Mtakatifu. Je, si Paulo alisema kuwa mmoja wetu asithubutu kupeleka ja—jambo mahakamani, kwa mahakimu dhalimu, kwa kuwa "hamjui ya kuwa Watakatifu watauhukumu ulimwengu?" Tutaketi na Kristo na kuhukumu wafalme na makuhani, na kuwahukumu watu hawa tuliowahubiri na kuwaambia wao kuhusu ule ubatizo wa Roho Mtakatifu nao wakakataa kuupokea. Wazia hilo!

59 La, hawakupotea, lakini hawatakuwa kamwe katika yule Bibi-arusi. Watafufuka katika ule ufufuo wa pili, bali hawatakuwa katika Bibi-arusi, na wahukumiwe kulingana na vile walivyoitendea Nuru waliyoipokea. Sasa, sehemu hiyo itakuwa juu ya Kristo. Ingawaje, hawakupotea.

141. Ndugu Branham, katika I Wakorintho—Wakorintho sura ya 14, kifungu cha 34 na 35, inasema, "Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena." Cha 35, "Maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa." Sasa, mwanamke aliye na nywele fupi aki—akinena kwa lugha ma—makanisani, kanisani, je, ni Roho wa—wa Roho Mtakatifu anayenena kupitia kwake au ni roho wa udanganyifu?

60 Sasa una...Na hili ni swali gumu sana, na naweza tu kujibu vema nijuavyo, waona. Sasa, singeamua, kwa sababu sikutumwa niamue. Lakini nadhani kuna wakati mwingi... Nina swali lingine hapa chini mahali fulani linaloambatana na hilo. Lakini kama mtu ananena kwa lugha, wametiwa upako na Mungu. Waona? Huenda wakawa nje ya taratibu, labda hilo ni kweli, nao huenda wanafanya jambo ambalo si sahihi, lakini singependa kusema kuwa haikuwa Roho Mtakatifu, kwa sababu singejua. Waona?

61 Na sasa kuna wakati mwingi ambapo hili ni . . . ambapo watu huamua kwa kosa wao kwa wao. Na ni jambo baya kufanya hivyo. Mwasema, "Naam, yeye ana nywele fupi, yeye anavaa nguo ambayo ni fupi sana, huyo—huyo—huyo si Roho Mtakatifu juu yake." Msifanye hivyo! Msifanye hivyo, hivyo si sahihi. Hujui ni nini kilicho katika moyo wa mwanamke huyo. Hujui lo lote kuhusu hilo. Unajua kuwa Roho Mtakatifu angemfanya awe na adabu njema kidogo, naam, huenda hilo likawa ni kweli. Lakini nitawaambieni, wewe na mimi hebu tumwachie Mungu aamue juu ya hilo. Na hebu Wewe na mimi tumwombee mtu huyo kuwa Mungu atawaonyesha wao Nuru.

62 Hapa wakati mfupi uliopita mtu mmoja alikutana nami nje hapa, kando. Nami nilikuwa na mpiga kinanda hapa aliyekuwa na rinda ndogo, fupi, ndogo, na hilo hasa halikuwa, nadhani, sahihi. Na mwanamke yule alikuwa na nywele fupi, naye alikuwa tu mchanga katika Njia hii, naye alikuwa akipiga piano. Na mtu fulani akakutana nami nje pale na akaanza kunishambulia sana, akisema, "Nawe u mhubiri wa kipentekoste, na unamruhusu mwanamke huyo kuketi juu pale! Hizo nywele fupi!" Na kuendelea kama cho chote kile.

63 "Vema," nilisema, "nadhani mwanamke huyo ana roho njema ndani yake. Hakika sikubaliani na hilo, mwajua, habari za rinda juu hapa, vile vipande viwili."

64 Kimoja kiko chini *hapa* na kingine kiko *hapa* juu ni kama shati wavaayo. Na kwa hivyo ni nyembamba sana na ilionyesha mavazi ya ndani waliyo nayo mle. Sidhani hilo—hilo lapaswa kufanywa. Si—sipendi hilo, hakika sipendi. Si—siwezi kusema, huenda wakawa tu wamejazwa Roho kama mtu mwingine ye yote, sijui; Mungu hujua hilo. Lakini singemhukumu mwanamke huyo na kusema kuwa yeye anaenda kuzimuni, kwa kumwangalia.

65 Mtu yuyu huyu alikuwa na bibi kanisani mwake aliyekuwa na nywele ndefu na alivalia nguo ndefu, na alikuwa na hasira ya kutosha kupigana na msumeno uvumao, na duni kupindukia. Naam, nywele ndefu na rinda ndefu hazikupeleki Mbinguni. La, bwana! Ni Roho aliye ndani yako akupelekaye Mbinguni. Bali ikiwa wewe kama Mkristo . . .

66 Ndiposa yakupasa ukumbuke kuwa wakati mwingi wachungaji hawataji mambo hayo nao watu wanaendelea wenyewe, wakidhani hilo ni sahihi. Lakini mchungaji yampasa hakika kuingilia hayo. Na—na—na ndipo dada wale wa kanisa, wale dada walio na tabia njema, wanaovalia mavazi yao vizuri, yapasa wawe vielelezo vya uzuri, na—na wawe kama mama na kama dada.

67 Nadhani kuwa mwanamke ye yote ambaye ni kama mama na mcha Mungu na ni kama dada apaswa kumwendea mtu kama huyo, na kwa uzuri wa Roho, aketi tu na kuongea na huyo

bibi. Na kama yeye ni wa Mungu, Roho Mtakatifu atafahamu mambo hayo, naye atajisahihisha. Lakini unapomlaumu upesi sana na kumfukuza, huenda ukamdhuru huyo mtoto mchanga, aliyezaliwa. Waona? Kwa hivyo si—singemlaumu mtu huyo.

68 Sasa, mtu kunena kwa lugha.

69 Sasa, si—sina budi kusema kitu fulani hapa ambacho huenda ni kigeni kidogo, na msipokubaliana nami, hilo ni sawa. Mwaona, sisi mara nyingi huhukumu mambo haya kwa kosa. Hebu kila mara tujaribu kuwazia mema sana juu ya mtu ye yote anayejaribu kufanya yaliyo mema. Hebu tuonyeshe wema wetu wote kwao. Lo, wanajaribu. Hatujui mioyo yao, isipokuwa una upambanuzi. Na kama wamekosea, ndipo ukiwa . . . Biblia ilisema, "Ndugu akighafilika katika kosa lo lote, hebu wale walio wa Roho wamwendee ndugu huyo kwa roho wa upole, wakijiangalia nafsi zao wasije wakajaribiwa wao wenyewe, uone iwapo huwezi kumpatanisha mtu huyo, waona, arejee kwa Mungu." Usiseme kuwa hawana roho wa kweli, kwa sababu . . .

70 Sikiza, sasa nitasema kitu fulani ambacho kitawachoma kwa dakika moja hivi, kwa hivyo tulieni kwa muda mchache. Roho Mtakatifu aweza kunena kupitia kwa mnafiki. Hakika! Nimeona yakitendeka, nami naweza kuwathibitishieni kwa Maandiko kuwa hiyo ni sawa. Naweza kuwathibitishieni kwa Maandiko kwamba nguvu za pepo huchukua roho hizo na kuzitumia, hakika, wanazichukua hizo karama na kuzitumia. Nimesimama papo . . . na kuona pepo wakinena kwa lugha na kufasiri. Nami nimeona wanafiki wakichukua Roho Mtakatifu halisi na kunena kwake. Hiyo ndiyo sababu huwezi kusema kuwa kunena kwa lugha ndiyo ishara pekee ya Roho Mtakatifu.

71 Sasa, wakati mdogo uliopita nilipoletwa mara ya kwanza katika Pentekoste, nilienda Mishawaka kwa maskani ya Ndugu Rowe. Pale walikuwa na mkutano, walikuwa ni watu wa Jina la Yesu. Sasa, sikukubaliana na watu wa Jina la Yesu, hakuna—hakuna . . . Wao ni ndugu zangu, lakini sababu nasema . . .

72 "Batiza kwa ajili ya *kuzaliwa mara ya pili,* katika Jina la Yesu Kristo," siamini hilo. Siamini kuwa maji hukuokoa dhambini. Naamini Damu ya Yesu Kristo ndiyo kuzaliwa mara ya pili. Lakini watu wa Oneness hubatiza kwa kuzaliwa mara ya pili. Jina la Yesu, ni, "Batizwa kwa Jina la Yesu, na hivyo umeokoka, kwa sababu yeye alisema, 'Tubuni mkabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu."

73 Lakini lipi laja kwanza? Toba, huzuni ya Kiungu kwa ajili ya dhambi zako, ndipo ugeuke. Kisha ubatizwe kwa Jina la Yesu Kristo, ni sawa. Mmefanya haya *yote* kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu.

74 Sasa, na ndani mle, kulikuwa na watu elfu kadha. Katika siku hizo kulikuwa na ubaguzi Kaskazini hapa, au Kusini, nao iliwalazimu kuufanyia humu kwa sababu ndugu wengi

weusi wangehudhuria mkutano huu. Ilikuwa P. A. ya W. na P. A. ya G. . . J. C. kabla hazijaugana. Na walikuwako kule Mishawaka, weusi na weupe, wote pamoja, hawangeufanyia kule Kusini wakati huo. Vema, niliona watu weupe wawili wameketi kitini. Nilikuwa sijawahi kusikia cho chote Juu ya Jumbe hizi hapo mbeleni maishani mwangu. Na pale watu wale wangesimama na mmoja angenena kwa lugha na mwingine angefasiri, na kuwaambia watu wale papo hapo mkutanoni shida zao, kuwaambia hao watu yale waliyokuwa wamefanya. Ndipo huyu angenena na mwingine angefasiri. Niliwaza, "Lo, nimeingia humu kati ya malaika." Sikuwa nimewahi kusikia jambo kama hilo!

75 Usiku wote, katika shamba la mahindi, naliomba. Kwa maana tangu mtoto mchanga, niliamini ya kwamba karama na mwito havina majuto, mimi kila mara nimeweza kuona maono. Na asubuhi iliyofuata wao waliniuliza nizungumze, nami nikafanya hivyo. Kule nje kulikuwa watu wengi walionijia na kunialika mikutanoni mwao, bali nilikuwa Mmishenari Mbatisti. Kwa hivyo nili—niliendelea mbele na kuyaachilia hivyo. Baada ya muda mfupi nilikuwa na hamu ku—kuwapata hawa watu malaika wawili. Sijapata kamwe kusikia cho chote. . .

76 Wangegeuka weupe midomoni, na kuinuka na kunena kwa lugha. Kisha yule mwingine angesimama wima na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, 'Juma hapa, yeye alifanya jambo *fulani,* hivi majuzi. Ulipotembea karibu na nyumba zile ulipata kijitabu cha mfukoni ambacho ni mali ya mtu huyu, mtu huyu alikipoteza hapa.' BWANA ASEMA HIVI, 'Kirudishe!'"

77 "Mungu, unirehemu, kiko hapa."

78 Waona, kweli, kusema tu kama hayo, kuwatambua watu moja kwa moja, nilidhani, "Lo, jamani, si ajabu hiyo!" Kwa hivyo, basi niliwaza, "Huyu ni Mungu!"

79 Vema, ndipo nikampata mmoja wa wale watu, na nilipokuwa nikiongea naye, niliomba, "Mungu, niruhusu mimi niwe nalo hata liwe ni nini." Sikujua nikiite nini, maona, sikujua nikiite nini. Na ndiposa kitu kile kilipokuja mbele yangu, nami nilipomtazamisha, niliendelea tu kuongea naye hata nilipoipata roho yake, kama tu vile yule mwanamke alivyofanya kwenye. . . Yesu alivyofanya, yule mwanamke kisimani. Tuliendelea tu kuongea hata nilipopata roho yake. Naye alikuwa Mkristo halisi, mtakatifu wa Mungu kweli kweli. Nikawaza, "Jina la Bwana libarikiwe!"

80 Nilikutana na—nilikutana na yule mtu mwingine pale pembeni, akija yapata nusu saa baadaye nami nikaongea naye. Na kama niliwahi kuongea na mnafiki, yeye alikuwa mmoja wao. Mkewe alikuwa na nywele nyeusi, naye alikuwa akiishi na mwingine mwenye nywele ya shaba nyeupe na amezaa watoto

wawili naye; na huku ananena na Roho yule yule mtu huyu alikuwa akinena kwake; na kutoa tafsiri ile ile, sawa hasa. Basi nikajua.

81 Kabla kuongoka kwangu, nilipata hakika ya mambo wakati mmoja nilipoingia katika kambi ya wachawi pamoja na Wahindi. Wao ni wacheza na pepo. Huchukua nyoka wakajizungushia, na kufanya ngoma ya mavuno ya mahindi, na kunena kwa lugha na kuifasiri, na kusema kweli yale hasa yaliyo kati ya watu. Na nikaona mchawi akichukua ka—kalamu na kuiweka chini, nikaona kalamu hiyo ikiinuka na kuandika kwa lugha, na kuifasiri na kuwaambia watu hasa yale yaliyokuwa yakiendelea pale pote. Katika mkutano wa wenye kunena na mizimu.

82 Kwa hivyo nilisema, mwaona, "Nimeingia kati ya pepo." nami nikaachilia hayo yote yaendelee.

83 Kwa hivyo siku moja pale Green's Mill, nilikuwa kule juu nikiomba katika pango langu, si kwa ajili ya hayo, nami nilitoka nje na kuweka Biblia yangu chini. Mimi. . . Koga mle pangoni hata na nikataka nuru kidogo ya jua, na ilikuwa alasiri, nami nilitoka nje na kuweka Biblia yangu chini. Nilikuwa nataka kusoma kidogo, nje pale kwenye gogo lililoanguka kuelekea chini ya kilima kila. Nami niliweka tu Biblia chini, nami nikaanza kuisoma. Na upepo ukavuma, na kuivumisha hata Waebrania sura ya 6. Niliwaza, "Labda Bwana ataka nisome hayo." Nikayasoma.

84 Kwa maana sisi tuliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, kwa kuwa tunaanguka, kujifanya upya tena hata tukatubu. Mvua huzaa . . . nchi huzaa mboga nayo mvua hutumwa kuzitia maji, na miiba na magugu hukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa." Kitu kama hicho.

85 Vema niliiisoma na kuwaza "Vema Bwana asifiwe." Nikagenza ukurasa mwingine, nikawaza Vema, nitasoma tu mahali fulani ndani hapa mahali pengine." Nikaiweka chini hivyo na kupangusa macho yangu upepo ule ulivumisha tena hata kwenye Waebrania 6 tena. Vema, hayo yalitendeka mara tatu au nne, mara tatu hivi, kwa vyo vote. Niliwaza, "Sioni ubaya wo wote hapo. Kuna nini mle?"

86 Hebu mimi ni, mwaweza. . . Mmeisoma mara nyingi, Waebrania 6, "Miiba na magugu. Mvua huinyeshea nchi mara kwa mara, kuilima, mnaona, kwa ajili ya matunda yake. Bali miiba na magugu hukataliwa hatimaye yakateketezwa, hukusanywa na kuteketezwa."

87 Singepata cho chote toka kwa hayo. Niliwaza, "Vema, miiba na magugu zitateketezwa, Mungu hukusanya Ngano Yake ghalani, na hilo latosha." Kasema, "Sioni chochote kuhusu hayo."

88 Nilikuwa nimeketi pale, nilikuwa nikitazama nje hivyo, na ono likaja mbele yangu. Nami nikaona dunia ikizungukazunguka hivi, na yote imelimwa tayari kwa kupandwa. Na mtu aliyevalia joho leupe, kichwa kimeinamishwa kwenye mfuko wa malisho, au mfuko wa mbegu, hasa, naye alikuwa akienda. Nami sijui kama ye yote wenu anakumbuka ule utaritibu wa kale wa kutawanya, jinsi mna . . . Nilimwona baba akifanya hivyo. Akizitawanya kwa mikono hivyo, na zingeanguka tu ardhini, hizo mbegu hivyo. Vema, mtu huyu alikuwa akipanda mbegu hivyo. Na mara tu yeye alipotoweka, mle juu nyuma yake ngano ikaanza kumea.

89 Vema, mara tu yeye alipozunguka mpindiko wa dunia, niliona kitu fulani cheusi kikija, kama mwezi mweusi. Nami nilitazama, nacho kikakaribia, ilikuwa m—mtu, mweusi kabisa, amevalia mavazi meusi. Yeye alikuwa akiotea, akitazama *hivi*. Naye alikuwa na mfuko wa mbegu, isipokuwa, ndani mle, yeye alikuwa na makwekwe. Naye alikuwa akiyapanda kati ya hii ngano *hivyo*, akiyatupa upande mmoja na ule mwingine. Na nyuma yake kukaota makwekwe, miiba, michongoma, magugu, na kadhalika.

90 Vema, niliwaza, “Hiyo ni aibu kwa mtu huyo kufanya jambo kama hilo.” Katika ono, sikuwa nikiliwaza kuwa la Kimaandiko, waona. Nami nilisema, “Yule mtu anapanda makwekwe katika shamba la ngano la yule mtu mwingine.”

91 Ndipo kukawa joto sana. Maskini ile ngano ikainua kichwa chake na kuenda, “hee; hee; hee,” hivyo, ikihema hivi ipate pumzi. Maskini lile gugu likainamisha kichwa chake, “hee, hee, hee,” lilikuwa likihema kwa maji, pia. Kila mtu aliomba kwa ajili ya mvua.

92 Baadaye ikawa . . . Wingu kubwa la ngurumo likaja na ikanyesha kote chini, na ilipofanya hivyo, mvua ikanyeshea nchi. Maskini ile ngano ikaanza kuruka juu chini, ikipaza sauti, “Haleluya! Bwana asifiwe! Haleluya! Bwana asifiwe! Na maskini yale magugu yakapasa sauti, “Bwana asifiwe,” yakainuka, uhai ukarudia yale magugu kama tu vile ngano.

93 Ndiposa Maandiko yakaja, “Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki.” Ndipo nikalipata. Mwaona?

94 Hili, kama mtu fulani anaketi makutanoni, roho anaweza kumshukia mtu huyo, na hali unajua wako makosani na hawaishi maisha mema, jihadhari yale usemayo kuhusu roho huyo, huenda ikawa ni Roho Mtakatifu. Usihukumu hu—huyo roho kwa mtu yule. Mtu yule huenda ni mkosiji lakini, sasa, si Biblia husema, “Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki?” Je, si Yesu alisema, mashamba yalipopandwa, “Viacheni vyote vikue pamoja, magugu na ngano, pamoja. Msijaribu kung’oa magugu. Msijaribu kuvihukumu, viacheni tu vikue pamoja. Na siku hiyo malaika watapelekwa na watayakusanya magugu yote

na kuyateketeza, na ile Ngano itakusanywa ghalani?" Lakini kwa matunda yao tunawajua. Unaweza kujua moyoni mwako. Zidi kujaribu kushughulika na mtu huyo.

95 Msiseme kuwa mwanamke huyu, kama yeye amevalia kizinifu au. . . Ilisomekaje? "Hebu tuseme kuwa Roho Mtakatifu atazuru. . . " Hebu tuone. La, nimepata lisilo hapa, sijui vipi. Lo, ndilo hili hapa, naam.

> **Wanawake wakinena kwa lugha. Sasa, mwanamke mwenye nywele fupi akinena kwa lugha kanisani, ni roho. . . Hebu tuone. Je, ni Roho wa Roho Mtakatifu anayenena kupitia kwake au ni roho wa udanganyifu?**

96 Mwaona, si-ngesema lo lote. Na kama ulidhani mwanamke yule hakuwa sahihi kwa kuwa na nywele fupi-. . . (naamini kuwa jambo ndilo hilo). . . naam, "nywele fupi," mbona wewe ndugu, kama wewe u mwanamume uliyeoa na huyu ni mwanamke aliyeolewa, mbona—mbona usiende na mkeo au umwambie mke wako aongee vizuri na maskini bibi huyu? Hebu tuamini yeye ana Roho Mtakatifu. Kama yeye yuko katika kanisa hili, ni—nitaamini ya kwamba yeye anaye. Halafu, sema tu, labda yeye ana. . .

97 Je, mlijua, mara kwa mara, huenda tukachunguzwa na kuonekana huenda ikawa sisi tuna kasoro fulani, pia. Mwajua, hi—hivyo ndivyo hasa. Kwa hiyo mtu fulani huenda akalazimika kutwambia kitu fulani. Mara nyingi watu wameniambia mambo mengi ambayo yalikuwa si sahihi, ambayo nilikuwa nikifanya, nathamini hilo.

98 Lakini hebu tuseme kuwa. . . hebu tuamini kuwa cho chote kile, hebu tuamini hili, kama mwanamke huyo si Mkristo hasa, kama anajifanya tu, Mungu atamhukumia hilo. Hiyo ni kweli. Lakini. . . Na kama yeye amevalia kizinzi, na mambo anayofanya si sahihi, Mungu atashughulikia hayo. Lakini hebu tuamini kuwa Roho huyo juu ya mwanamke huyo ni Roho Mtakatifu. Mwaona, kwa sababu hatujui.

99 Sasa, kama tafsiri ya huyo roho mtakatifu inatoa jambo fulani, laana kwa Kristo. . . "Hakuna mtu anayenena kwa Roho, husema, Kristo amelaaniwa." Kama mwanamke huyo yuanena kwa lugha na tafsiri ije kuwa "Kristo amelaaniwa," ndipo unajua huyo ni pepo mchafu juu ya mwanamke yule. Lakini mradi tu anambariki na kumtukuza Kristo, basi amini Roho huyo. Waona? Amina. Natumai hayo hayatatanishi. Natumai hiyo inatoa nuru ndogo juu ya hilo, kwa vyo vyote.

142. Kumbukumbu la Torati, sura ya 23, na kifungu cha pili, si inafundisha kuwa mtu aliyezaliwa nje ya ndoa hawezi kuokoka? Yasema kuwa "Mungu atawapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne." Eleza maana yake.

100 Vema. Uzinzi ulikuwa kitu kibaya mno katika siku za Biblia hata kama mtu alipata mtoto kwa mwanamke ambaye hakuwa mke wake, mtoto huyo, watoto wa mjukuu wake, kwa vizazi vinne, miaka mia nne na kitu, hawangeingia hata katika makutano ya Bwana, sababu ni kwamba damu ya fahali na mbuzi na ndama haikutosha kuondoa dhambi. Ingetenga tu dhambi, au ingefunika tu dhambi. Haingeondoa dhambi. Waona? Haingeondoa dhambi, ingefunika tu dhambi. Uzinzi ni tendo baya mno!

101 Mwanamke, kito cha thamani, ambaye Mungu amemwumba yeye kuwa mama, amempa wajibu wa umama, kwamba akizaa mtoto kwa mtu mwingine asiye mume wake, basi kulikuwa na laana juu ya mtoto huyo, na watoto wake, na watoto wake, na watoto wake kwa vizazi vitatu na vinne. Hata mara nyingi vitu kama kaswende, na—na upofu na mengineyo yuliwaambukiza watu. Naam, lilikuwa tendo baya, tendo baya mno kwa mwanamke kuwa na mtoto nje ya ndoa takatifu. Sasa, si wakati huo tu, bali bado ni jambo baya mno, hakika ni baya, kila mara.

143. Je, Ezekieli 38 na 39 itatimia kabla ya Kunyakuliwa.

102 Sasa kama utachunguza, Ezekieli 38 na 39 hushughulika na Gogu na Magogu, ambayo ni Urusi, ile nchi ya kaskazini. Sasa, sisemi hili ni sahihi, lakini kwa njia yangu ya kufundisha hilo, kwamba, itatimia baada ya Kunyakuliwa, baada ya Kanisa kutwaliwa. Na Mungu atashughulika na Gogu na Magogu watakapowakabili Israeli pale. Nami nadhani hilo litatimia baada ya Kunyakuliwa. Sasa, hilo haliifanyi kuwa hivyo, waona. Lakini hivyo ndivyo ninavyofundisha hayo. Nadhani hilo ndilo walilotaka kujua, wazo langu lilikuwa nini.

144. Bwana ametwambia kwa unabii kuwashuhudia wengine mambo ambayo tumesikia na kuyaona hapa, kama kukaribia kwa kule Kuja, ubatizo katika lile Jina, katika Jina la Yesu, na mambo kama hayo. Tumewaambia mambo haya wengine ambao wanaonekana kuwa Wakristo, bali haionekani kama wanaamini. Je, wewe wadhani nini kitatendeka kwa watu hao? Je, watanyakuliwa?

103 Sasa, ninashukuru uliuliza hivyo, "Wadhani nini?" Ambayo haitaifanya sahihi kwa sababu ningewaza hilo. Naamini hakuna mtu awezaye kutembea katika Nuru ya Mungu hata Mungu atakapomfunulia Hiyo. Nami siamini kuwa mtu ye yote ambaye. . .Mambo haya yote yaliyofichika yamefichwa kwa watu, na hakuna mtu awezaye kuyaona isipokuwa Mungu awafunulie, nami naamini hivyo kwa sababu katika Biblia imekuwa hivyo daima.

104 Si Yesu alisema kuwa "Mna macho na hamwezi kuona, mna masikio na hamsikii?"

105 Na hali katika Mathayo, naamini ni sura ya 8 au ya 12, ilisema kuwa "Ijapokuwa Yesu alikuwa amefanya miujiza mingi mbele yao, bali hawangeamini. Kwa sababu Isaya alisema, unabii ulisema kwamba Wana macho na hawaoni, na masikio na hawasikii.'" Mwaona?

106 Naye Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipoitwa na Baba Yangu kwanza, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Hilo latosheleza, mwaona.

107 Sasa, una—una wajibu wa kueneza Nuru, si wajibu wako katika kupokea kwao ile Nuru. Ni wajibu wako kuipeleka kwao, lakini katika lile watendalo kwayo. Ndiposa Mungu akiwaingiza, hilo litakuwa juu Yake. Kama hawajavalia mavazi, na kadhalika, nao hawafanyi. . .Lakini wao. . .Kumbuka, hawawezi kuiona hata Mungu awafunulie.

145. Ndugu Branham, katika Danieli sura ya 11, kifungu cha 31, inafundisha kuhusu siku kule. . .kuondolewa kwa sadaka ya kuteketezwa ya kila siku, na chukizo la uharibifu. Je, waweza kueleza haya ni nini?

108 Lo, mtu huyu ameandika jina lake kwa hili. Hilo ndilo somo langu Jumapili ijayo, na hilo linaambatana na yale—na Majuma Sabini ya Danieli. Lakini. . .Na huenda nikasema tu haya kwenu, ndugu yangu mpendwa uliyeandika jina hapa, ambaye ni rafiki mpendwa sana kwetu sisi sote. Naam, "lile chukizo la uharibifu," Yesu, katika Mathayo 24, alinena kulihusu. Chukizo (maana yake ni uchafu) la uharibifu, lile chukizo lilikuwa ule Msikiti wa Kiislamu wa Omar uliojengwa katika uwanja wa lile hekalu ambapo palikuwa Patakatifu.

109 Katika A.D. 96, Tito aliingia na kuuteka Yerusalemu na kuteketeza hekalu lile, nao wakajenga ule Msikiti wa Omar (Ile dini ya Kiislamu) papo hapo kwenye uwanja wa hekalu lile, na bado ungalipo pale hata wa leo. Na utakaa pale hata Mungu atakapowarudia Wayahudi tena. "Na lile chukizo (hilo ni ule Msikiti wa Omar) la uharibifu wa Patakatifu," limesimama katika mahali Patakatifu, waona.

110 Yesu aliirejea, na kusema katika parandesi "(asomaye na afahamu)." Mwaona? Kwa hivyo, alitoa siku nyingi sana, toka wakati huo hata yule. . .baada ya yule Mtawala na siku nyingi sana na kadhalika, ambazo tutaziingilia Jumapili yayo. Na nitajaribu, vizuri nifuavyo, kupata hilo kwa ajili yako Jumapili ijayo. Lakini hili chukizo ni Msikiti wa Omar ulio chukua mahali pa hekalu, ambalo, "Hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu lile lilionenwa na nabii Danieli, limesimama katika Mahali Patakatifu." Mwaona, likisimama mahali ambapo hekalu lilisimama (Mali Patakatifu), Msikiti wa Omar.

146. Ndugu Branham, je, hujisikii kuwa kila mmoja anayedai kuwa Mkristo apaswa kulipa fungu la kumi, kulipa fungu

la kumi lao katika ghala ya Bwana? Tafadhali toa Andiko kwa swali hili.

111 Vema, mkitaka . . . Hiyo ni kweli, basi Biblia ilisema katika Malaki, sura ya 4, "Je! mwanadamu atamwimbia Mungu? Nanyi mwasema, 'Tumekuibia kwa namna gani?' Mmeniibia zaka na dhabihu. Leteni zaka kamili ghalani Mwangu, mkanijaribu," asema Bwana, "kama sitawafungulia madirisha ya Mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha kuipokea."

112 Hilo ni himizo kwa mtu ye yote! Laiti ningekuwa na wakati, na singefikia tu Andiko hili ndogo ninalotarajia kuliingilia yapata dakika kumi zijazo, ningetaka kuwatoleeni ninyi ushuhuda wa kibinafsi jinsi hata nilikuwa na njaa, na mama yangu na wengineo walikuwa na njaa, na baba yangu mgonjwa, lakini nilitoa fungu langu la kumi kwanza na kumtolea Mungu, na laiti ungeona yale yaliyotendeka. Sijawahi kuona maishani mwangu, mwanamume ye yote au mwanamke, ambaye, hata kama unapata tu dolla moja kwa juma, utaleta senti kumi ya pesa hizo na uweke ghalani mwako, au kanisa unaloshiriki, Mungu asipoibariki hiyo uniite mimi mnafiki. Naam, bwana. Hilo ni himizo kwa ye yote. Na kila Mkristo . . . Hilo laenda kwa swali hili lingine. Kila Mkristo apaswa kutoa fungu la kumi! Hiyo ni kweli. Lapasa kutolewa.

Vema, sasa:

147. Mtu au watu wakinena kwa lugha zisizojulikana katika usawa wa sauti kila wakati, jambo lile lile, lakini tafsiri ni tofauti kwa mfasiri kila wakati, je, huyo aweza kuwa Roho Mtakatifu?

Sasa hebu nisome hilo tena:

Mtu au watu wakinena kwa lugha zisizojulikana katika usawa wa sauti (yaani, kunena tu kitu kile kama neno fulani tena na tena na tena) **kila wakati, na kitu kile kile kila wakati, lakini tafsiri ya mfasiri ni tofauti kila wakati, je huyo aweza kuwa Roho Mtakatifu?**

113 Naam, hilo ni gumu, lakini hebu nitoe nuru kidogo tu kwake nikiweza. Nami nina hakika mtafahamu kuwa huyu ni Ndugu Branham tu nikijaribu kufanya vema kadiri niwezavyo, lakini hebu tu nieleze hili kwa ujuzi wangu binafsi katika kushughulikia mambo ya kiroho. Nami nathamini matumaini yenu kwangu kwa kuniuliza maswali kama haya. Kama hamngenisadiki mimi, hamngeniuliza hayo. Naamini Mkristo hangeuliza swali kuzusha ubishi, naamini wanajaribu kupata Ukweli. Mwaona? Nami ningejibu, na kama . . . Na nitalijibu, na iwapo nimejieleza dhahiri "ni kadiri nijuavyo," ndiposa kama roho huyo aliye ndani yako akikasirika, hilo laonyesha si Roho Mtakatifu aliye ndani. Waona? Kwa hivyo basi Roho

Mtakatifu hatakasirika, atasahihishwa kila wakati kwa Neno, na atastahimili kusahihishwa.

114 Sasa hebu niseme hili, kuwa mimi . . . Katika hali hii, kumbuka, Mungu awe hakimu wangu. Mimi, huyu ni William Branham, singesema. Lakini katika ujuzi niliopata kwa kushuhudia huku nikiwa chini ya upako wa mikutano kama hiyo, naamini kuwa mtu yule anayesema jambo lile tena na tena kila wakati, usawa ule ule wa sauti, hakika yuanena kwa lugha. Naamini, ninaamini, kuwa Roho wananena kwa lugha, kama wao ni Wakristo. Wananena kwa lugha, bila shaka. Lakini naamini unapata fasiri iliyo kombo.

115 Sasa, wakati mwingi, watu . . . na—nataka . . . Nadhani ni watu tu wa kanisa hapa, nadhani, usiku huu, kwa vyo vyote, karibu wote. Sivyo, Ndugu Neville, ni karibu tu wale wanaohudhuria? Kwa hivyo wageni wakiwa ndani humu na unatofautiana na hili, ninajaribu kunena kwa kanisa langu mwenyewe, mwaona.

116 Sasa, kama baba yenu katika Injili, kama m—mchungaji wenu, ningependa baadaye kidogo, wakati roho zenu na karama zinapoanza kufikia ukamilifu . . . Mkianza kuziona zikianza kulegea na kuwa . . . basi heri umchunge—chunga mtu yule, acha tu yapite kwa sababu si Roho wa Mungu juu yao. Lakini wanapokuwa wazuri na wapole na wanyenyekevu na tayari, na kila kitu, huyo ni Roho wa Mungu. Na kama—kama mtu fulani akienda nje ya taratibu na mchungaji ajaribu kumrekebisha, na roho yule aruke juu, basi si Roho wa Mungu. Roho wa Mungu kila mara husimama, huja kwa Neno. Mwaona? Hutambua Neno kila wakati.

117 Sasa, lakini sasa mimi sijaribu ku—ku—kusifu isivyostahili au kudhoofisha. Mimi najaribu tu kusema kweli. Sasa, mtu fulani akinena kwa lugha, na mwingine asimame na kufasiri lugha. Sasa sikizeni kwa makini. (Na nadhani haya yananaswa. Sivyo?) Katika kufasiri lugha . . . Sasa nitaingia katika mafundisho fulani sasa kwa hili. Katika kufasiri kwa lugha, watu wengi hufasiri lugha kwa kujisikia kusiko kwa kawaida wakijisikia waseme jambo kama hilo. Hiyo si kufasiri.

118 Kufasiri ni wakati wanaponena katika lugha isiyojulikana, unaisikia katika Kiswahili na kurudia tu yale wanayosema. Lakini . . . kama mtu huyo anena katika kanisa lenu . . . Sidhani tunayo katika kanisa hili. Kama yako, sijayasikia.

119 Lakini mtu fulani akisimama na kusema neno fulani, tena na tena, au usawa wa sauti na kuendelea, kuendelea, kuendelea, kuendelea . . .

120 Nawaambieni, siamini Junie Jackson yuko hapa usiku huu. Yuko? Sidhani yeye yuko. Lakini kila siku nimeshangaaa kuhusu Junior Jackson na kunena kwake kwa lugha, na Ndugu Higginbotham, na wengi wenu hapa, jinsi mnavyoona huko

kugeuzwa kwa sauti katika kufasiri. Mwaona? Sasa—sasa hilo ni sawa. Sasa, si . . . sijivunii kanisa langu. La, bwana. Ikiwa kanisa langu lahitaji sahihisho, ni—nitasimama hapa na kufanya niwezavyo kwa ajili ya Mwokozi wangu, hiyo ni kweli, liudhi lisiudhi. Mimi—mimi ni baba yenu katika Injili, mwaona, nami nataka . . . Hamtaki roho mbaya, mnataka roho wa kweli. Ninyi nyote mnataka hivyo . . .

121 Mbona uchukue—uchukue badilisho hali anga zote za Pentekoste zimejaa yaliyo halisi? Mbona ule katika pipa la taka hali kuna meza nzuri, kubwa, safi, imeandaliwa hapa na kuku na maandazi na kila kitu? Waona? Mbona tungefanya hivyo? Mwaona? Hebu tupate ile halisi, hiyo ndiyo tunayotaka, ile iliyo halisi sana.

122 Sasa, naamini, katika matamshi haya yaliyotamkwa hapa, kitu kile kile tena, naamini katika matamshi hayo kuwa yote ni sahihi, lakini siamini kuwa mwenye kufasiri anafasiri lugha ya mtu yule. Siamini hayo. Naamini Roho yupo na mfasiri anatabiri. Naamimi yeye ni mtabiri badala ya mfasiri ikiwa yeye hasikii sauti hiyo katika lugha yake . . . ? . . . "Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu kwa lugha yetu tuliyozaliwa nayo?" Mwaona, yakupasa usikie vivyo hivyo, yakupasa usikie katika Kiswahili. Kama . . .

123 Hapa, huyu hapa *mfasiri*. Sasa, naweza kusimama, nami na—najua maneno mawili au matatu katika—katika—katika lugha nyingine, ninayoiyajua. Sasa nachukua tu hili vivi hivi tu, si kwa kiroho sasa. Sasa nitasema, "Baie, baie bly. I . . . Ekke wil Afrikaans Sprekken." Sasa, sidhani kunaye mtu humu anayejua yale niliyosema. Naam, ndugu, nilisemaje? [Ndugu katika makutano asema, "Ulisema ungenena Kiafrikana,"—Mh.] Kiafrikana, "Baie, baie bly," "Nina furaha tele." "Mimi niko hapa kunena Kiafrikana" mwaona, "Afrikaan Sprekken." Mwaona?" Mimi niko hapa kunena Kifrikana."

124 Sasa, yeye alifanyaje? Yeye . . . Nilikuwa nikinena Kiafrikana lakini yeye alinielewa katika Kiswahili. Hiyo si kweli? Kwa sababu unajua Kiafrikana. Sasa, kama unanena . . . kama ninasimama hapa au ninasema . . . ninahubiri, na Ndugu Neville anafasiri kwa lugha nyingine ya watu, yeye anasema kwa lugha yao yale anayosikia nikisema; yeye ajua yale ninayonena kwa sababu yeye ajua lugha yangu.

125 Na kama unanena kwa lugha isiyojulikana, na kufasiri, unasikia katika lugha uliyozaliwa nayo, kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kufasiri yale wanayosema, kwa sababu Roho Mtakatifu ameifasiri kwako na wewe unanena tu kwa Roho Mtakatifu.

126 Lakini basi kama Roho yupo kumbariki maskini mtu huyu, nao wanasimama . . . Kama ndugu mpendwa mzee, Mungu, yeye yuko Utukufuni usiku huu, naamini bila shaka. Mzee

mpendwa sana nimjuaye, Ndugu Ryan, sisi sote tulimjua. Yeye alikuwa akisimama pale barabarani . . . (Na Mungu, anisamehe, si ati nakufuru, . . . najua ni . . . Kumkufuru Roho Mtakatifu hakusameheki.) Lakini Ndugu Ryan alizoea kusema neno moja tena na tena wakati wote, kitu kama "Sekeem na sekeem," au kitu kama hicho. Naye alikuwa na . . . Naam, mtu fulani alisema, "Je, wadhani hayo ni ya Mungu?"

127 Nilisema, "Bila shaka, ni ya Mungu! Bila shaka, naamini ni ya Mungu." Lakini yeye alikuwa akinena kwa lugha, bali singesema yale yeye alikuwa akisema kwa sababu sijui. Lakini, uwepo wa Roho ulikuwepo.

128 Kwa hivyo kama uwepo wa Roho uko, na mtu huyu anasema tu neno moja, tena na tena, na tena, na huyu mwingine aruke juu na kujaribu kufasiri, hali yeye hajui yale yule anasema. Kama mtu huyu hafasiri, yeye anatabiri, roho wa unabii yu juu yake na yeye anatabiri, si kufasiri.

129 Kwa hivyo, Mkristo mpendwa, kwako uliyesema kuwa, "Je, huyo aweza kuwa Roho Mtakatifu?" Huenda ikawa ni Roho Mtakatifu akitumia afisi mbili. Moja, ikibariki mtu kwa kunena kwa lugha; na ile nyingine, ikitabiri sio eti kufasiri yale yule anayosema. Bali yeye aliyanena. Roho Mtakatifu alikuja juu yake katika unabii wakati ule ule ambapo huyu alikuwa akinena kwa lugha, naye alidhani ilikuwa ni tafsiri, tofauti yake ni nini? Ni Roho wa Mungu akitoa ujumbe kwa kanisa. Lakini *kufasiri,* yakupasa ufahamu katika Kiswahili na urudie hasa yale mtu yule aliyosema, hiyo ndiyo karama ya kufasiri.

148. Kama kuna—kama kuna jumbe tatu tayari zimetolewa katika lugha zisizojulikana katika mkutano mmoja, basi je, katika mstari wa kuombea wagonjwa kwaweza kuwa na jumbe zaidi zilizotolewa na iwe katika utaratibu wa kiroho wa mkutano ule?

130 Naam, bila shaka. Naam. Hakika. Ninajua unakoelekea. Paulo hapa kasema, "Kama kulikuwa na . . . Mnahutubu na kunena kwa lugha," kitu fulani kama hicho, Paulo akinena . . .

131 Baadaye kidogo, ninyi nyote mnapo . . . Ndugu Neville, nyote mnapotaka kuja sasa, watu hawa walio na karama za kiroho . . . Sasa, kama mtatumaini ujuzi wangu wa Maandiko, nitakuja mkutanoni pamoja nanyi watu pekee mlio na hizi karama, pamoja nanyi nyote pekee, ili tuketi pamoja . . . Na mkijisikia . . . Nawe chunguza, Ndugu Neville, na uone kanisani, kwamba ni Mungu na ni Mungu akitenda kazi kati yao, hilo ndilo tunataka, lakini tunataka kuweka hilo katika taratibu ili lipate kubariki kanisa na kufanya kitu fulani. Mimi . . . Mungu si . . . najua, naam, najua yale Maandiko, la kufanya. Na hilo ndilo tunalotaka kufanya.

132 Sasa, mtu huyu hapa, najua, naam, najua ananena kwa lugha, yapaswa kuwa kwa zamu, wawili, au isizidi watatu. Hilo ni sawa, lakini kama mtatambua hapa, kama ilikuwa . . .

133 Kama tu mtu fulami atupe pale . . . Kama Ndugu Sothmann aliinuka na kutoa ujumbe katika unabii au kunena kwa lugha. Kufasiri lugha ni unabii, mwaona, roho wa unabii. Sasa, ukinena tu kwa lugha isiyonjulikana, kusiweko fasiri, mtu yule anabarikiwa na Roho, lakini yeye hadhuru kanisa.

134 Sasa, yale Paulo alikuwa akijaribu kufikia ni haya, "Mnatumia ibada yote kwa kunena kwa lugha, mwaona, na mtu mjinga kasema, 'Haya—haya ni nini, kwa vyo vyote?'" Mwaona, wao hawafahamu isipokuwa kuna kufasiriwa. Na kuweko . . . kuwe na jumbe moja mbili au tatu katika mkutano.

135 Sasa, mtu yule hapa asema, "Basi katika mstari wa wanaohitaji maombi?" Hilo halina budi kuwa kwamba labda mtu fulani katika mstari wa wanaohitaji maombi . . . Labda, Ndugu Neville, au katika kanisa lingine au ko kote litokako, ya kwamba katika mstari wa wanaohitaji maombi mtu huyu . . . au katika mikutano ya uponyaji wa Kiungu, huenda ilikuwa katika mikutano ya Ndugu Roberts, mkutano wa Ndugu Allen, au wengineo, katika mkutano wangu au mtu mwingine, sijui. Lakini, si hoja, yale Paulo ananena ni kuhusu ujumbe kwa mkutano kule nje, "Hebu wale wawe watatu tu," kwa sababu ujumbe wa Mungu unanena ujumbe fulani ukijaribu kuutoa kwa kusanyiko. Lakini wakati mtu yule yuko katika mstari wa wanaohitaji maombi, yeye anatabiria mtu binafsi, si wote. Kama ndivyo ilivyo, nimekuwa nje ya utaratibu kote katika mstari wangu wa wanaohitaji maombi, mwaona, wanapokuwa thelathini au arobaini usiku mmoja? Waona, kama unamtolea unabii mtu binafsi.

136 Lakini mtu huyu anatolea unabii mwili wote, hebu pawe jumbe mbili au tatu na kisha zikome. Ijapokuwa Roho Mtakatifu huenda akataka kunena, lakini ngoja kidogo, lipe Neno nafasi leendelee. Mwaona? Ndiposa, hasa, kunena huko kwapaswa kuwe kabla au baada ya Neno, hakuna lo lote lipaswalo kukatiza Neno linapoanza kutolewa. Lakini, hata hivyo, tutaweka hilo katika utaratibu baadaye wakati roho na karama zitakapoanza kukamilika.

137 Tunaongea sasa juu—juu ya uzito wa Kanisa la kipentekoste, namaanisha Kanisa halisi la kipentekoste. Nasi tuna furaha kuwa Mungu yungali anaishi na kutawala na kunena kupitia kwetu.

138 Sasa, lakini kama, kwa mfano, kama dada hapa angetoa ujumbe kwa lugha au atabiri, na bibi anayemfuata angetoa ujumbe kwa lugha au atabiri, na kisha bibi aliye karibu naye au mtu fulani nyuma kule, mtu fulani atatoa ujumbe au atabiri, au lugha. Bila shaka karibu wote wananena kuhusu jambo lile

lile, kama Mungu ana haraka, akijaribu kunena jambo fulani, akiwaita watu fulani binafsi kanisani wafanye kitu fulani, sasa, au kitu fulani ambacho Yeye anataka kifanywe.

139 Sasa basi, kwa mfano, mstari wa wanaohitaji maombi ufanywe, na Ndugu Neville au mimi mwenyewe au mhuduma mwingine ye yote amwendee mtu huyu binafsi, hiyo si kwa mwili ule, hiyo ni kwa mtu huyu binafsi. Na Roho wa Mungu aja juu yake kumwambia huyu mtu jambo fulani, ndipo amwambie, kwa sababu yeye haneni kwa kusanyiko. Yeye anamzungumzia mtu huyu binafsi, si kusanyiko, kwa hivyo hilo ni sawa.

149. Vema, Mpendwa Ndugu Branham, mara kwa mara Bwana hunionyesha mimi vitu katika ndoto. Yeye amenionyesha mimi vitu kuhusu mwanangu katika jeshi la wanamaji, ambavyo mwanangu aliniambia vilikuwa "siri." Yeye amenionyesha vifo vya watu pamoja na siri za mioyo ya watu. Je, hii ni karama toka kwa Mungu? Yeye anionyeshapo katika ndoto, mioyo na nia za watu, kila kitu daima kimetendeka jinsi tu ndoto hunionyesha.

140 Naam, ndiyo, ndugu yangu au dada, ye yote yule. Bwana akubariki. Hiyo ni, nionavyo mimi, karama ya Mungu. Ni karama ya Mungu. Hamjui Biblia yanena kuhusu ndoto? Yusufu, jinsi yeye alivyoota ndoto na kuzifasiri, na jinsi wengine waliota ndoto. Vitu hivyo ni vya Mungu. Sasa, kama ni vya Mungu, kila mara vitakuwa kweli, kila mara zitatendeka vivyo hivyo hasa jinsi Yeye alivyosema.

141 Na sasa msi. . . Ukianza kujivunia hiyo, itaondoka. Waona, kuwa tu mwenye kicho na mzuri. Na Yeye akuonyeshapo lo lote, na ni kitu fulani kikupasacho kumwambia mtu fulani, kuwa wamefanya kitu fulani kibaya, basi usiinuke na kumkemea mtu yule, waendee wewe mwenyewe na kusema, "Dada, ndugu, wajua, Bwana aliniambia usiku uliopita kuwa—kuwa ulikuwa ukifanya kitu fulani kibaya, jambo *fulani*."

142 Kama mtu huyo akisema, "Umekosea! Huo ni uongo! Sikufanya hilo!"

143 Sasa, jambo la kufanya basi ni kurudi na kusema, "Baba wa Mbinguni, je, hilo lilikuna makosa?"

144 Sasa, kama mtu huyo. . . Ndipo kama mtu huyo alikuwa akikwambia kweli, basi una roho mbaya. Lakini kama mtu yule alikuwa akisema uongo, na yeye alifanya hivyo, Mungu atamshughulikia mtu huyo. Waona? Naam, bwana. Kwa sababu, waona, yale yeye amefanya pale, yeye amemkufuru Roho Mtakatifu, akikana yale Roho Mtakatifu amemwonyesha. Waona, kwa hivyo ni jambo baya.

150. Ndugu Branham, inawezekanaje ka—kanisa kucheza, kupasa sauti, kunena kwa lugha, na kuacha Roho. . . (hebu tuone, sasa ngoja kidogo) **. . . na kuwa katika Roho, sana, na iwe vigumu sana kwao kusoma Maandiko. Silifahamu.**

145 Wala nami pia, "kupiga kelele, kucheza, kunena kwa lugha, na hata wasisome Maandiko." Ni—ni—ninasema hili, kumbukeni ni, William Branham, ambaye angekosea kwa maili milioni moja. Naamini watu wengi sana . . . Niliulizwa swali hilo leo na ndugu fulani, kitu fulani kama hicho. Ya kwamba, wanapoenda kuombea wagonjwa, ndugu fulani atamwombea mmoja, kisha awafanye wote waimbe au kucheza katika Roho, akidhani hilo huleta nguvu kati ya watu. La, kwa—kwangu mimi, naamini hilo ni kosa.

146 Naamini kuwa mtu anapokuja katika mkutano wa uponyaji itakuwa kama anapokuja apate wokovu, aje kwa kicho, akiamini. Kila mtu ndani mle, si kupiga kelele na kucheza, lakini wakimwona ndugu yao au dada akielekea kule kumuomba Mungu rehema, inamisheni vichwa vyenu na muanze kuomba, "Mungu, msaidie ndugu yangu sasa mchungaji anapomwombea, anapompaka mafuta. Na Roho Mtakatifu aje juu yake na ampe imani kuamini kwa uponyaji wake. Yeye ni ndugu mpendwa. Yeye ni dada mpendwa." Mwombeeni badala ya kuimba tu, kupiga kelele na kucheza.

147 Lakini twaona mengi sana ya hayo katika mikutano yetu ya Kipentekoste, ni kila wakati . . . Naamini ni kuabudu, hakika naamini wanamwabudu Mungu. Naam, bwana. Naamini hilo kwa moyo wangu wote. Nami naamini katika kunena kwa lugha, kupiga kelele na kucheza. Nami naamini kila sehemu yake, naam. Naamini lo lote wanalofanya katika Biblia ni zuri tu leo kama lilivyokuwa wakati huo, bila shaka, lakini naamini lina wakati wake na taratibu yake.

148 Sasa, kama baraka kuu imeanza, na watu wanapiga kelele, na utukufu wa Bwana una—unashuka, na watu wanataka kupaza sauti sana na kupiga kelele na kufanya lo lote Roho analowaambia. Endelea, hiyo ni sawa. Lakini mtu ajapo kuponywa, ambapo ni jambo kati ya mauti na uzima, naamini yatupasa tuwe watulivu na kuongea na Baba na kunena Naye kwa ajili ya ndugu huyu. Badala ya kumwabudu, hebu tumwombe, "Baba, Mimi—mimi ni mwabudu Wako. Nakupenda, Wewe wajua nakupenda, naonyesha upendo wangu Kwako. Sasa naonyesha imani yangu Kwako, msaidie ndugu yangu apone. Utafanya hivyo, Baba?" Naamini mtapata matokeo bora kwa kufanya hivyo. Bila shaka naamini hivyo. Na kumcha Roho wa Mungu.

149 Lo, haya huenda yamekosea maili mia lakini natumai nimeyajibu, hilo ni, kuchochea—kuangazia Nuru zaidi. Najua yaliyo niani mwenu sasa, kwa vyo vyote. Nami hebu niwaambieni, baadaye kidogo nataka kumwuliza mchungaji hapa kama atakuja anisaidie ku . . . labda aje humu na awakusanye watu wote pamoja walio na Roho wa Mungu juu yao katika karama, na tuongee juu yake kwa muda mchache. Labda naweza kuwasaidieni mpande ngazi juu zaidi na kumkaribia

Mungu kwake...na kuziweka zaidi kwa taratibu kanisani. Nimekuwa nikichunguza kote, yaonekana ajabu kwangu. Nami napenda tu kuiona ikiendelea na kuendelea, na kuendelea na kuendelea.

150 Na tunapoinuka juu, msimkubalie Shetani ajipenyeze, sasa. Wee, yeye ni mjanja. Mm! usimshinde kwa akili, usijaribu kufanya hivyo, kwa sababu huwezi. Mtegemee tu Mungu, na uendelee tu kutembea kwa unyenyekevu, na Mungu atafanya hilo, na utaona ya kuwa Mungu atakutumia wewe zaidi na zaidi na zaidi hivyo. Bwana awabariki.

151 Je, tuna wakati wa kuongea dakika ishirini? [Makutano wasema, "Amina!"—Mh.] Asanteni. Asanteni. Nadhani hayo yalikuwa ya kutosha kuniamsha, Ben. Vema.

152 Hebu tugeukie Zaburi kwa muda mchache. Yaonekana Bwana alikuwa akinipa wazo ndogo hapa ambalo ningetaka kuwaelezeni ninyi nyote usiku huu kama mahubiri, mkitaka, kwa dakika cha—chache tu. Najua kuna joto, na kuna joto humu, pia. Lakini, hatutakutana tena, labda, hadi Tumatano usiku. Kwa hivyo hebu tusubiri tu na—na kabla hatujaimba ule wimbo mzuri wa zamani wa *Heri Kifungo Kitufungacho,* hebu—hebu tuongee kuhusu lile—lile Neno lililoandikwa. Maswali haya yanatufanya sisi...yanatuacha wenye wasiwasi. Hebu—hebu tuyaache sasa, na—na kunena katika Neno.

Sasa twaweza kuinamisha vichwa vyetu tena kwa muda tu:

153 Baba wa Mbinguni, maswali haya, nimejaribu kupata yale watu hawa wanayo mioyoni mwao, kuona kama watauliza kuhusu *hili* na kuhusu *lile*. Naona, Bwana, wanatamani karama za kiroho. Na wale walio na karama za kiroho wanashangaa wazitumieje. Kwa wengine, inatoa Nuru kuu kwa kanisa; kwa wengine wanashangaa. Sasa, Bwana, tusaidie. Tusaidie, Bwana. Sisi ni watoto Wako. Sisi hatufanyi mambo haya kujiheshimu wenyewe, tunafanya haya kwa kumheshimu Mungu kwa kipawa kile Mungu ametupa sisi.

154 Twaomba, Baba, kuwa utabariki karama hizi na kuzidhihirisha kanisani. Na iwe ya kwamba wasafiri na wageni, wanaotuzuru, wanaoingia kule mlangoni na kuketi chini dakika chache, na Roho wa Mungu awe mkuu sana humu ndani hata atatujulisha siri za kila moyo uingiao mlangoni mle. Tujalie, Bwana. Na iwe katika uzuri sana na unyenyekevu, si kwa ukali na kukemea na kuvunja-vunja. Twajua Roho wa Mungu sivyo alivyo.

155 Kwa hivyo twaomba kuwa utatubariki sisi katika kila kitu. Bariki kanisa letu, bariki watu wetu. Bariki watu wa makanisa yale mengine. Pia, Baba, twajua kuwa kunalo Kanisa moja pekee na sisi sote tumezaliwa katika Hilo.

156 Nami naomba, Baba, kuwa utatubariki tena ninaposoma hili fungu ndogo ambalo yaonekana ulinipa, nikiketi pale kwenye

dawati alasiri ya leo. Pia nisaidie, Bwana, nisiwakawishe watu sana, lakini kunena tu matamshi machache hapa. Nami naomba ya kwamba utakuwa ndani yake. Na utupe wazo ndogo, ambalo twaweza kuenda nyumbani nalo na kumshukuru Bwana kwa uzuri Wake. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

157 Sasa, msisahau, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda.

158 Sasa fungueni Zaburi 106, na kifungu cha 7. Ningesoma zaidi, sehemu . . . sehemu ya Zaburi hii. Lakini, ni Daudi. Kusudi la kunijia, ilikuwa kwa ajili ya ujumbe wa asubuhi hii. Na, nitaweka saa yangu hapa na kujaribu kuondoka saa tatu na nusu, ikiwezekana. Sasa kwenye kifungu cha 7 cha Zaburi 106;

> *Baba zetu katika Misri Hawakufikiri matendo yako ya ajabu; Hawakukumbuka wingi wa fadhili zako; Wakaasi penye bahari, . . . bahari ya Shamu.*

159 Nitasoma kifungu kinachofuata:

> *Lakini akawaokoa kwa ajili ya jina Lake, Ayadhihirishe matendo yake makuu.*

Bwana aongeze baraka Zake.

160 Nitawazungumzia, Bwana akipenda, juu ya somo la *kutoelewa;* Mungu, akikosa kufahamika. Nitalichukua hivyo: *Mungu Akifahamika Vibaya.*

161 Mwajua, kutoelewa vizuri hutuingiza katika shida nyingi. Wakati mwingi watu husema mambo ambayo wanakariri toka kwa mtu mwingine, ambaye, wao hawakumwelewa. Hilo humwingiza mtu katika shida. Naamini ingekuwa vema kwetu tukiwa tu, vema, tungoje hata tuelewe yale tuliyokuwa tukinena. Si mnadhani hivyo? Najua ingekuwa, kwangu, jambo nzuri kwangu mimi kuchunguza kwanza, na kisha kusema hivyo. Waona? Bali kila wakati twaonekana kuwa tusiofahamika. Na hapa Daudi ananena kuhusu Israeli, walikosa kufahamu miujiza Yake walipokuwa Misri.

162 Sasa, kukosa kufahamu si kusema tu, "Vema, sikusikia yale aliyosema," lakini kuona kitu fulani kikifanywa na *usijue ni cha nini.* Hilo ni . . . Hilo ni kukosa lengo lote kabisa basi.

163 Sasa, Mungu hafanyi muijiza kusema tu, "Mnaona, mimi ni Mungu." Mungu hufanya muujiza ili afahamike. Mwaona? Mungu huifanya kwa kusudi fulani. Na mliona kusomwa kwa Zaburi hapa katika hiki kifungu cha 7? Nadhani ni kizuri sana, nataka kukisoma tena:

> *Baba zetu katika Misri Hawakufikiri matendo yako ya ajabu;* (mwaona, walikosa kuyafahamu) . . . *hawakukumbuka wingi wa fadhili zako; wakaasi penye bahari hata, . . . bahari ya Shamu.*
>
> *Lakini akawaokoa kwa ajili ya jina lake, ayadhihirishe matendo yake makuu.*

164 Mnaona, walikosa kufahamu kwa nini Mungu, kule Misri, alitenda miujiza hii. Yeye alikuwa akijaribu kuwaonyesha rehema Zake. Yeye alikuwa akijaribu kuwafanya wafahamu kuwa Yeye alikuwa Mungu kati yao. Napenda hilo.

165 Katika mahubiri yangu madogo niliyoyahubiri hapa hivi majuzi, kule Chicago, halafu naamini niliyahubiri hapa, wale wavulana waliyanasa kwa kanda, *Kama Tai avurugavyo Kiota Chake*, anapapatika juu ya makinda yake. Jinsi yule mama tai huwatwaa makinda yake madogo. . . Kabla hajawapurukusha, wana manyoya mengi sana yaliyolegea. Nao hawajamwona vizuri kwa sababu yote huwa yanachuchumaa kiotani. Bali yeye huruka juu ya kiota na kunyosha mabawa yake makubwa na yenye ngunu. Yuafanya nini? Yeye anapaza sauti, anataka wajue sauti yake. Ananyosha mbawa zake kubwa.

166 Tai wa kike wakati mwingine ndiye huwa mkubwa zaidi. Inasemekana kuwa tai wakati mwingine, wa kike ndio wakubwa, wana mbawa urefu wa futi kumi na nne kutoka ncha hadi ncha, humnyakua ndama na kuruka naye. Futi kumi na nne, kutoka ncha hadi ncha. Mbawa hizo, zina urefu wa jukwaa hili papa hapa, toka mwimo hadi mwimo.

167 Yeye hufika pale mbele ya huyu kida mdogo kwa sababu gani? Yeye yuaenda kumpurukusha. Yeye hata hajawahi kuwa nje ya hicho kiota. Naye anampeleka juu angani kisha anamtikise amtoke, amwachilia juu kule apapatike mwenyewe, ajifunze kupuruka. Kwa hivyo yeye ataka kuonyesha mamlaka aliyo nayo. Yeye hunyosha mbawa zake kubwa apate kuegemeza manyoya, naye anapaza sauti, na ndipo anawapungia hewa. Lo, jamani! Manyoya yanarushwa toka kiotani na kadhalika, yeye anapungia upepo ndani mle kama eropleni. Anatupwa chini chali, naye hulala chali, kisha hutazama juu na kuwaza, "Mama, jinsi wewe ulivyo mkuu! Jinsi wewe ulivyo mkuu!"

168 "Umeona jinsi mbawa zangu zilivyo na nguvu? Naweza kukuinua juu na kukupeleka mahali po pote ninapotaka. Nina nguvu!"

169 Na hivyo ndivyo Mungu alikuwa akiwafanyia Israeli. Mwajua, Yeye alisema, "Kama tai avurugavyo kiota chake," ni jambo lile lile. Yeye aliwapata Israeli kule katika nchi ya kilio, kisha akamleta Misri na kumpeleka katika ile nchi ya ahadi, juu ya mbawa za tai. Mwaona? Basi Mungu alikuwa akifanya miujiza hii kwa nini? Yeye alikuwa akijaribu kuwaeleza watu Wake kuwa Yeye alikuwa Yehova mwenye nguvu.

170 Na hayo ndiyo Yeye anajaribu kufanya leo! Yeye haponyi watu eti kwa sababu Yeye aweza kuponya. Yeye yuajaribu kukujulisha ya kwamba Yeye ndiye Ufufuo, ya kwamba Yeye aweza kukuponya, Yeye aweza kuufufua mwili wako. Yeye aweza kufanya lo lote atakalo, Yeye ni Yehova! Napenda hilo.

171 Lakini watu walikosa kumfahamu. Mungu ni rahisi sana kutofahamika na wasioamini, kwa wale wasiotaka kufahamu. (Watu wengi hujaribu kufahamu.) Wengi hawataki kufahamu, wao hujifungia tu wenyewe, na kusema, “Hakuna kitu kama hicho,” na “Siamini mambo kama hayo.” Basi hawawezi kufahamu kamwe.

172 Lakini mtu anayetaka kufahamu, aliye tayari kuketi chini (“Haya, njoni, tusemezane,” asema Bwana) sasa, mtu yule yu—yuko kwenye njia ya kujifunza kitu fulani toka kwa Bwana. Lakini watu ambao kila mara wanachangamana na Mungu na nguvu za Mungu...Ni vigumu kuchangana na Mungu bila kuchangamamana na nguvu Zake, kwa sababu unapochangamana naye unafahamikiana naye, au una uhusiano Naye, ndiposa una nguvu Zake ndani yako.

173 Hiyo ndiyo sababu watu hawawezi kuamini miujiza leo, kwa sababu hawana cho chote ndani yao cha kuaminia. Yawapasa wawe na kitu fulani ndani mle kuaminia. Na Roho wa Mungu awapo ndani ya mwanadamu, yeye atasema “amina” kwa kila Neno la Mungu na kila muujiza wa Mungu. Lakini kama mama yangu alivyozoea kusema, “Huwezi kupata damu toka kwa mboga nyekundu, kwa sababu haina damu.” Kwa hivyo hivyo ndivyo ilivyo, huwezi kupata kuamini toka kwa asiyeamini, kwa sababu hakuna cho chote mle cha kuaminia.

174 Mtu fulani alisema, “Siamini uponyaji wa Kiungu, haidhuru ungesema nini.” Hakika, hayo si kwa ajili yake, ni kwa ajili tu ya wale wanaweza kuamini. Kama utapata damu ipate kutoka kwa kitu kilicho na damu. Kama utapata imani, ipate toka kwa kitu chenye imani.

175 Na hivyo ndivyo Mungu hutumia kitu kilicho na imani. Yeye hakutumi nje hapa katika mkutano wa uponyaji kama huna imani ya kutosha kuamini. Yeye atakutumaje nje kwa mkutano wa kufanya miujiza kama huna imani ya kutosha kuiamini? Yeye anataka kitu kilicho na kitu fulani ndani mle ambacho Yeye aweza kutumia kupata kitu fulani. Kwa hivyo watu walikosa kufahamu.

176 Nuhu alikosa kufahamika kabisa katika siku zake. Nuhu, aliyejuana na Mungu, mtumishi wa Mungu, mwamini katika Mungu. Na unapokuwa mtu anayeamini Mungu unafanya mambo kinyume kabisa na yale watu hudhani ni sahihi hata wanadhani kuwa una wazimu. Na Nuhu, alipoonywa na Mungu, alitayarisha safina kwa ajili ya wokovu wa nyumba yake. Na watu walidhani yeye alikuwa wazimu. Yeye hakuwa wazimu, yeye alikosa tu kufahamika kwa sababu alikuwa akifuata uongozi wa Mungu. Amina! Napenda hilo. Yeye alikosa kufahamika.

177 “Mtu angewezaje hata...” Mnasema, “Hamna mvua iliyopata kutoka angani. Mvua ni nini?” Haikuwa imenyesha

kamwe, Mungu alinyunyizia ardhi maji. “Nuhu, iko wapi mvua hiyo?”

“Sijui.”

“Nionyeshe iko wapi!”

“Siwezi kukuonyesha.”

178 “Vema, unajuaje itanyesha toka huko juu ambako hamna yo yote kule ya kunyesha?”

179 Nuhu huenda alisema kitu kama hiki, “Mungu aliniambia itanyesha. Na kama Mungu alisema ‘Itanyesha,’ Yeye aweza kuipeleka kule juu kisha aimwage.” Amina. Hilo latosha. Kama Mungu alisema hivyo, ni hivyo tu. Waona? Yeye alikosa kufahamika kwa sababu alikuwa akimfuata Mungu.

180 Eliya. Ningekaa kwa somo hili wakati mrefu, lakini ninayo kadha hapa ningetaka kuyafikia upesi. Eliya alikosa kufahamika na taifa lake. Eliya alikuwa Mwisraeli, yeye alikuwa Myahudi, naye alikosa kufahamika kwa sababu kila mara alikuwa akilaumu taifa lake, akimlaumu mfalme, akimlaumu malkia, akilaumu kila kitu kilichokuweko. Na kuvilaumu! Jinsi alivyoonekana kuwa mwenye kisirani. Naam, jamani kila kitu, kilikuja “BWANA ASEMA HIVI. Mungu atakuadhibu, ewe Yezebeli, ewe *fulani*.”

181 Yeye alikosa kufahamika. Kwanini? Yeye alikuwa akimfuata Mungu. Haikuwa Eliya ambaye walikosa kufahamu, ilikuwa kutenda kazi kwa Roho Mtakatifu katika Eliya ambako hawakufahamu.

182 Mtu angewezaje kuinuka dhidi ya taifa lake? Akakufuru taifa lake, akilisahihisha, na kuweka laana ya Mungu juu yake, taifa lile lile, watu wale wale alioishi nao. Jamaa yake, rangi yake, kanuni yake ya imani, tabaka yake, na isitoshe akatabiri hukumu za Mungu na kuwaagizia njaa. Yeye alikosa kufahamika, kwa sababu haikuwa Eliya, ilikuwa Mungu katika Eliya ambaye hawakumfahamu. Haikuwa kutokufahamika kwa Eliya, ilikuwa Mungu akimwongoza Eliya, nao walikosa kufahamu kuwa Mungu alikuwa Mungu Mtakatifu na hawezi kuvumilia dhambi.

183 Na haidhuru kama ni ndugu yako, dada, au mama, haidhuru ni nani, ni dhambi machoni pa Mungu na hukumu itawajilia kwa ajili yake. Kufahamika vibaya.

184 Danieli alikosa kufahamika wakati wana wote wa Israeli walipoisujudu sanamu ile, bali yeye na Shedraki na Meshaki na Abednego walikataa kusujudu. Vema, wao walisema, “Ana nini huyu?” Taifa lote lilisema, “Kuna nini kwa huyu mtu mwenda wazimu? Vema, Waebrania wengine wote walimtambua Mungu wetu, walimtambua, wanamsujudu tunapopiga tarumbeta, na kupiga tarumbeta na kupiga zeze, na kadhalika, na kupiga zomari. Wote wanasujudu, lakini kuna nini kwa huyu mwenye

kisirani? Kuna nini kwake, yeye hatalifanya?" Kwa sababu yeye alikuwa anawasiliana na Mungu! Hivyo ndivyo ilikuwa. Yeye alikosa kufahamika. Yeye alidhaniwa kuwa "Wazimu, au hana akili. Vema, wao walikuwa kundi la wenye kisirani." Lakini wao walikuwa wakifuata tu uongozi wa Roho. Hiyo ndiyo sababu walikosa kufahamika.

185 Manabii wote wa Agano la Kale, jinsi walivyoinuka na kutabiri dhidi ya taifa lao, jinsi walitabiri dhidi ya watu, jinsi walivyotabiri dhidi ya kitu, hicho, wakiweka laana juu yao, na kufanya mambo kama hayo. Wao walikosa kufahamu. Kwa nini? Wao walikuwa watumishi wa Mungu, walikuwa wakifanya mapenzi ya Mungu, walikuwa katika huduma ya Mungu, kwa hivyo wao walikosa kufahamika.

186 Na ye yote anayemfuata Mungu hukosa kufahamika. Yesu, Bwana wetu, wakati wa kuzaliwa Kwake, Yeye alikosa kufahamika.

187 Wale mamajusi, hawakufahamika, walikuwa wakifuata ishara ya kimbinguni kumtafuta Mfalme aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi. Wao walijua kulikuwa na Nyota itakayoinuka toka kwa Yakobo, kulingana na unabii wa Danieli. Nao walijua Mfalme huyu atakuwa Mwokozi, Yeye atakuwa Mfalme wa Israeli. Nao walikuja kwa miaka miwili, kutoka India, kupitia Mto Tigris, na kuvuka jangwa na kupitia milimani, kila mahali, kisha wakaingia katika mji wa Yerusalemu jioni moja yapata machweo, wakipaza sauti, "Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Yuko wapi?"

188 Na hamna mtu aliyejua lo lote kuhusu hayo. Lilikuwa jambo la ajabu kwamba Mfame wa Wayahudi alizaliwa na watu waliokuwa umbali wa mamia ya maili walijua hayo; na papa hapa katika mji alikozaliwa, na mahali alipozaliwa, kati ya watu aliozaliwa kwao, bali hawakujua lo lote juu yake. Hawakuwafahamu mamajusi. Wao walisema, "Hakuna kitu kama Mfalme wa Wayahudi. Tuna mfalme juu hapa, Herode."

189 Yeye hakufahamika katika kuzaliwa Kwake alipozaliwa. Mariamu alikuwa mja mzito kabla hajaolewa na Yusufu. Alikosa kufahamika. Wao walidhani alizaliwa nje ya ndoa takatifu, hawakujua ya kwamba alichukua mimba ya mtoto huyu kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Lakini haikufahamika. Lilikuwa tendo la Mungu na watu wakakosa kulifahamu.

190 Wao bado hawalifahamu, tendo la Mungu kila mara halifahamiki.

191 Ni watu tu wanaoamini ya kiroho, watu wanaomwamini Roho. Lakini ilifahamika kwa kosa, wale Mamajusi walikosa kufahamika.

192 Herode hakulifahamu. Herode aliposema, "Vema, niambie aliko yule mtoto mchanga, nami nitaenda kumsujudu, pia." Yeye alikuwa mnafiki, alikuwa akisema uongo. Alichokuwa

anaogopa . . . Yeye hakujua Maandiko kuwa ilimpasa Masihi kuja, Mfalme wa Mbinguni. Basi Herode alidhani angekuwa mfalme wa dunia hii, naye alitaka kumwuua apate kumwangamiza.

193 Haikuwa mfalme wa dunia hii, Yeye alisema dunia hii si ufalme Wake, "Kama huu ulikuwa Ufalme Wangu raia Wangu wangenipigania, lakini Ufalme Wangu ni wa kule juu." Herode hakufahamu, yeye alidhani alikuwa mfalme wa dunia hii.

194 Hivyo ndivyo wanavyosema siku hizi, "U wa kanisa gani kama u Mkristo? Dhehebu gani?"

"Sina!"

195 Hawaelewi. Mwaona, hawawezi kufahamu. Wanadhani *dhehebu* maana yake ni "Mkristo." Ni vinginevyo. Hivyo hasa. Lakini haifahamiki na watu.

196 Sasa, twaona kuwa Herode alikosa kulifahamu, yeye hangefahamu.

197 Nikodemo hangeweza kufahamu, kule Kuzaliwa mara ya pili, alipomjia Yesu usiku. Mtu fulani alimlaumu. Simlaumu. Yeye alikuwa mtu mzuri, alitaka kujua jambo fulani. Yeye alikuwa ana shughuli nyingi siku nzima, labda alikuwa afisini mwa kuhani wake, au cho chote kile, ilimlazimu kuja usiku. Hata hivyo, yeye alifika pale, yeye alifanya vema sana kuliko watu wengi wafanyavyo sasa. Hawatakuja mchana *wala* usiku. Hatimaye akafika; kabla hujamlaumu, wewe umefika? Hatimaye akamwendea Yesu, na tusimlaumu, kama *sisi* hatujawahi kuwa kule. Na ikiwa umekuwa kule, basi sidhani ungemlaumu. La, yeye—yeye alifika kule. Naye alikuja usiku, na labda yeye alikuwa na shughuli nyingi. Hata hivyo, alikuja. Labda Yesu alikuwa na shughuli nyingi nje kule akiwaombea wagonjwa na kadhalika, wakati tu pekee yeye angempata kwa mahojiano haya ingekuwa usiku. Lakini mwishowe alifika kule akakaa pale hadi alipopata mahojiano na Yesu. Na Yesu aliposema . . . Yeye—yeye alisema, "Rabi, twajua kuwa Wewe u mtu uliyetumwa toka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu angefanya mambo haya uyafanyayo isipokuwa Mungu awe pamoja naye."

198 Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuingia katika Ufalme, hata hangeuona Ufalme."

199 Na yule mwalimu mkuu, mwalimu katika Israeli, alisema, "Mimi, mzee, kurudi tumboni mwa mama yangu na nizaliwe tena?" Mnaona, yeye alikosa kufahamu yale Yesu alikuwa akinena, hakuyafahamu. Kwa sababu Yesu alikuwa anaongea kuhusu Kuzaliwa kwa kiroho, naye alikuwa akijaribu kuyaweka kwa kuzaliwa kwa mwili. Kwa hivyo yeye hakufahamu Yeye, hakulipata. Yeye tu . . . jinsi watu wafanyavyo. Kama tu vile Nikodemo, wengi wetu hukosa kufahamu mambo ya Mungu kwa sababu tunayachukua tu na kuyaweka kwa mambo ya kawaida.

200 Kama, tuseme, daktari fulani aseme, “Lo, siamini uponyaji wa Kiungu. Siamini kuna kitu kama hicho.”

201 Nilimsikia daktari fulani akimwambia mwanamke fulani afisini wakati mmoja, kasema . . . Naye hakujua . . . Yeye alitaka kujua ilikuwaje kwa kile kivimbe alichokuwa nacho. Yeye kasema, “Ndugu Branham aliniombea kisha Bwana akaniponya.”

202 Yeye alisema, “Siliamini.” Yeye akasema, “Siwezi kamwe—siwezi kamwe kuamini jambo kama hilo.” Kasema, “Niambie nani aliyekiondoa.”

Kasema, “Tafuta kovu.”

Kasema, “Ulikiweka nini?”

203 Kasema, “Sikuweka cho chote kamwe.” “Yeye aliniita tu mkutanoni halafu kitu hicho kikaondoka.”

204 Nami nilikuwa nimeketi papo hapo katika chumba cha pili, naam, nimeketi chumba cha pili, nikisikiza. Mwanamke yule hakujua nilikuwa humo. Wala huyo daktari hakujua nilikuwa mle, kwa sababu hata yeye hakunijua, waona. Na nilikuwa nimeketi mle ndani. Naye alisema . . . Nikimpeleka mtu mwingine afisini mwa daktari. Hiyo ni kweli hasa. Nami nilitaka tu kusikia yale aliyokuwa akisema, nilimchukua—nilimchukua mgonjwa yule na kuondoka pale nilipotambua hilo, kuwa yeye hakuamini.

205 Kwa hivyo yeye alisema, “Siamini hata kidogo.” Kasema, “Sijawahi kamwe kuona cho chote ambacho kingefanya kitu kama hicho. Siamini hata.” Kasema, “Yapasa nilione kabla sijaliamini.”

Yeye akasema, “Vema, na kivimbe cha—changu je?”

Alijibu, “Yapasa nione kikiondoka kabla sijaamini hilo.”

206 Mwaona, kuona si kuamini. “Imani ni bayana ya mambo ambayo huyaoni!” Waona, unaamini kwanza ndiposa inatendeka. Kwa hivyo mtu yu—yule hakuwa mwamini, kwa hivyo basi yote yalikuwa siri kwake. Yeye hakujua aliyokuwa akinena kwa sababu yeye—yeye hangeyafahamu, yalikuwa fumbo kwake.

207 Watu husema leo, “Lo, siamini huo uponyaji wa Kiungu. Siamini Roho Mtakatifu huyo. Siamini huko kunena kwa lugha. Siamini kupiga kelele. Siamini upuzi huu wote hivyo. Siamini.” Kwa nini? Ni siri! Ni wewe tu unayefahamu vibaya. Ni Mungu, yako hapa katika Biblia. Ndiyo haya hapa yakitoa matokeo yale yale ambayo Biblia ilinena yatatoa, basi haina budi kuwa ni Mungu. Ni wewe tu unalifahamu, makosa hivyo tu. Mungu amekosa kufahamika.

208 Wanafunzi Wake hawangefahamu miujiza yake. Usiku huo Yeye alipoingia mtumbwini, kisha akasema, “Huyu ni mtu wa

namna gani hata pepo na bahari zamtii?" Walikosa kufahamu kuwa Yeye hakuwa mwanadamu, Yeye alikuwa Mungu.

209 Hiyo ndiyo shida ya watu leo, wanataka kumfanya Yeye mvulana wa kuleta bahati njema, kitu fulani kinachobeba vibao vya kuchezea mpira. Wanataka kumfanya Yeye mtu mdogo kambini.

210 Yeye hakuwa mtu mdogo kambini, Yeye alikuwa Yehova, Mungu! Hawakumfahamu. Walimtarajia Yeye kuwa mmoja wao, Yeye hakuwa mmoja wao, Yeye alikuwa Mungu kati yao! Yeye alikuwa zaidi ya mwanadamu. Kama vile ninavyosema mara nyingi, Yeye alikuwa mwanadamu alipoona njaa, lakini alikuwa Mungu alipowalisha elfu tano kwa biskuti, biskuti mbili na vipande vya samaki. Yeye alikuwa mwanadamu alipochoka kule mtumbwini, lakini Yeye alikuwa Mungu alipotuliza upepo na mawimbi na kuzifanya zimtii Yeye. "Huyu ni mtu wa namna gani?" Yeye hakuwa namna fulani ya mtu, alikuwa Mungu aliyedhihirishwa *katika* mtu. Hawakumfahamu. Wao walimdhania kuwa mtu, mwana wa Mariamu, seremala, lakini Yeye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Amina!

211 Askari wa Kirumi hawakumfahamu, walipompeleka mahakamani, na kufunga kitambaa machoni mwake, na kumpiga kichwani wakisema, "Sasa, kama Wewe ni nabii tabiri, watu wote husema Wewe ni nabii, njoo utwambie nani aliyekupiga kichwani."

212 Mnaona wao hawakufahamu kuwa Yesu alisema, "Nafanya tu yale Baba anionyeshayo niyafanye. Mimi hufanya yale anayonionyesha Baba, ndiposa nafanya yale Yeye ananiambia niyafanye." Hawakumfahamu, walikosa kufahamu huduma Yake.

213 Wayahudi hawakumfahamu. Jinsi Yeye alivyokuwa Rafiki na Mwokozi wao, nao walitaka kumfanya Yeye kitu kiovu. Walikosa kufahamu huduma Yake. Yeye alisema, "Malkia wa kusini atasimama Hukumuni na kizazi hiki na kukihukumu, kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia aisikie hekima ya Suleimani. Na hapa yupo aliye mkuu kuliko Suleimani." Lakini walikosa kufahamu ya kwamba Yeye alikuwa mkuu kuliko Suleimani. Wao walidhani Yeye alikuwa mtu tu.

214 Wengi wao walidhani Yeye alizaliwa nje ya ndoa takatifu, eti alitoka kwa jamaa baya iliyokuwa na tamaa hizi na mengineyo, na mtoto haramu. Naam, tayari tumekwisha kuwa na swali hilo, hata hawange-. . . Kwani wao walisema, "Hasha, twajua Wewe umezaliwa nje ya ndoa takatifu, una pepo. Je, unajaribu kutufundisha sisi? Sisi ni marabi!"

Yeye alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi."

215 Mnaona, walikosa kufahamu. Wakati wale askari wa Kirumi waliporudi wakati mmoja, wakimsikiza Yeye, kasema,

"Hajanena kamwe mtu ye yote kama huyu anavyonena. Hatujapata kusikia mtu akinena hivi."

216 Haikuwa mtu akinena, ilikuwa Mungu! Naam, bwana. Hajanena kamwe mtu kama. . . Mtu hufafanua na kunena Maandiko, Yesu huyafanya Maandiko *hai*. Mtu haishi hivi: "Maandiko yasema *hili* hapa, ndilo hili hapa!" Mtu aweza kusema, "Maandiko yasema hili," lakini hivyo tu ndivyo awezavyo kufanya. Lakini Yesu angesema, "Mimi na Baba yangu tu umoja, Baba Yangu yuaishi ndani Yangu. Aliyeniona Mimi amemwona Baba." Hakuna mwingine ye yote angelisema hayo! Amina. Haleluya! Hiyo ni kweli. "Aliyeniona Mimi amemwona Baba." Hakuna mwingine ye yote angelisema hivyo!

217 Si ajabu hao askari walisema, "Hajanena kamwe mtu ye yote kama huyu." Yeye haneni kama mwandishi au mhubiri, Yeye anena kwa mamlaka! Na hata pepo wanamtii, na upepo na mawimbi vinamtii. Wao walidhani Yeye alikuwa mwanadamu, lakini Yeye alikuwa Mungu.

218 Mnaona, Yeye hakufahamika. Kasema, "Hasha, Wewe—Wewe ulizaliwa mwana haramu. Ulizaliwa nje ya ndoa takatifu, nawe unajaribu kutufundish sisi? Naam, twajua Wewe u wazimu na una pepo. Wewe ni Msamaria, umekuwa kule na una pepo. Unajaribu kutufundisha sisi, marabi watakatifu?"

Yeye alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi."

219 Naam, walikosa kumfahamu, hawakujua Yeye alikuwa nani. Hiyo ndiyo shida siku hizi, watu wakijaribu kumfanya Yeye kitu fulani asicho. Yeye si mtu tu, Yeye ni Mungu katika mwanadamu! Si nafsi ya tatu, Yeye ndiye Nafsi pekee. Naam, bwana. Vema, hakika, walikosa kumfahamu.

220 Mafarisayo, yule Mfarisayo aliyemwalika chini kule wakati huo kwa chakula cha jioni, karamu kubwa, alikosa kumfahamu. Yeye alidhani angekuwa naye tu kule. Nilihubiri ujumbe huo hapa si muda mrefu umepita kwenye kiamsha kinywa, naamini, kule Chicago, kwenye kiamiha kinywa. Mfarisayo huyo alisema, "Sasa, mtazame Yeye ameketi kule nyuma, ameketi kule nyuma, hajaitawadha miguu na kadhalika. Maskini mwanamke yule aliingia na kumsafisha Yeye kwa machozi, na kumpangusa na nywele za kichwa chake." Yeye akasema, "Kama Yeye alikuwa nabii, angejua ni mwanamke wa namna gani anayemtawadha miguu. Yaonyesha Yeye si nabii!"

221 Yesu akasimama, akasema, "Simoni, nina neno ninalotaka kukwambia!" Amina, yeye hakufahamu, hivyo tu. Yeye alisema, "Mimi. . . Ulinialika Mimi nije, nami niliacha mipango yangu yenye shughuli nyingi kuja kwa mwaliko wako. Na wakati. . . Wewe hukunilaki mlangoni. Hujaitawadha miguu Yangu. Hukunipaka kichwa changu mafuta. Hukunikaribisha kwa busu. Uliacha tu niingie, mchafu na nikiwa na harufu mbaya na jasho tupu, kisha ukaniketisha hapa pembeni kunifanyia

mzaha. Bali huyu mwanamke, mwanamke *huyu*, yeye hakuacha kunibusu mfululizo miguu Yangu, naye ameiosha kwa machozi yake ya toba." (Ni maji mazuri jinsi gani!) "na kuipangusa na nywele za kichwa chake. Nina neno moja dhidi yako, Simoni. Amin, nakwambia, amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi." Simoni hakufahamu; yule mwanamke alifahamu. Simoni alisema, "Yeye ni mwanadamu tu"; Yeye alisema, "Yeye ni Mungu, Mwokozi wangu!" Yeye hakufahamika. Yeye bado hafahamiki.

222 Wanafunzi wale kule Kalvari, hawakumfahamu, wakati wote walipomkana na kuondoka. Wangemwonaje mtu, mtu waliyejua alifanya miujiza na kufufua wafu, hata hivyo ajitolee mwenyewe hata afe, kisha aondoke aende kule, apigwe, huku analia, mate yakitiririka usoni mwake, huku yamechanganyika na damu, hapo walipokuwa wameng'oa ndefu kadha, wakazing'oa usoni mwake; na kumpiga mijeledi mgongoni Mwake hata mifupa Yake ikajitokeza, wakampiga mateke, na kumpiga kila mahali; na askari watusi na walevi, wakampiga barbarani. "Na asimame na aache wao wafanye hivyo?" Hawakufahamu, kwa hivyo wao walisimama mbali. Hiyo ni kweli.

223 Shetani hakumfahamu. Shetani alisema, "Hakika huyu hawezi kuwa Mwana wa Mungu ambaye angesimama pale na kudhulumiwa hivyo, nao wakitusi, na wanafunzi wangu kule wamfanyie vyo vyote, naye anavumilia. Yeye si Mwana wa Mungu."

224 Pia Mafarisayo, makuhani, hawakumfahamu, kasema, "Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, jiokoe Mwenyewe toka pale."

225 Yule mwizi aliyekuwa upande wa kushoto hakumfahamu, yeye alisema, "Kama Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, tushushe toka msalabani, jiokoe nafsi yako na sisi pia."

226 Lakini yule mwizi aliyekuwa mkono wa kuume alimfahamu, yeye alisema, "Sisi, tumefanya maovu nasi tunastahili yale tunayopata, bali Mtu huyu hajatenda lo lote." "Bwana, nikumbuke utakapoingia katika Ufalme Wako!"

227 Tazama Sauti hiyo ikijibu, kasema, "Leo, utakuwa pamoja nami Paradiso." Yeye alifahamu kuwa huyo alikuwa Mungu akifa kwa ajili ya dhambi zetu. Njia pekee ambayo Yeye angekufa, ilikuwa auawe katika mwili. Yeye hawezi kuuawa katika Roho, kwa sababu Yeye ni Roho wa Milele. Naye alipaswa kuwa katika mwili kusudi apate kuuawa, kwa hivyo wao walimfahamu tu makosa. Yeye alifahamu.

228 Siku moja, yapata siku kumi baada ya hayo, au yapata siku arobaini baada ya hayo, ilikuwa siku hamsini, hao wanafunzi walipanda orofani, nao wakakaa mle juu kwa siku kumi mchana na usiku hata siku ya hamsini ilipotimia. Ndipo, kwa ghafula,

kukaja uvumi toka Mbinguni kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi. Kwa sababu Yesu alikuwa amewaambia, “Tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini kaeni mjini Yerusalemu, hata mvikwe Uwezo utokao Juu.” Walijua kuwa utakuja. Walijua ingetukia, haina budi kutendeka. “Nendeni kule juu mkakae hata nizitume.” Wao wakakaa kule juu. Waliungama, wakaondoa kila kitu katika nia na mioyoni mwao. Walikuwa wakingoja, wote katika nia moja, mahali pamoja, wakingoja ile Ahadi; wakitembea hapa na pale, wanaume kwa wanawake, wakitembea-tembea kule juu pamoja orofani, huku milango imefungwa ili Wayahudi wasiingie na—na kuwadhuru.

229 Kwa ghafula, walikuwa kule juu wakitembea-tembea, na kukaja toka Mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukavuma mle, kisha ndimi za Moto zikaanza kuwakalia wao. Milango ikafunguka, madirisha yakafunguka, wakaenda nje barabarani.

230 Nao walikosa kufahamika, hata wakasema, “Si hawa watu wamejawa na mvinyo mpya? Watu hawa wamelewa kwa sababu tunawasikia wakigugumiza maneno, hatujui yale wanayonena.” Kwa ghafula, wao wakasema, “Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu wenyewe, si hawa wote ni Wagalilaya?” Hawakufahamu kwamba ilikuwa ahadi ya Baba.

231 Ndipo Mungu alikuwa na nabii pale ambaye angesimama na kunena, Petro akasema, “Enyi watu wa Yerusalemu nanyi mnaokaa Uyahudi, msikose kufahamu haya. Haya ndiyo yale yaliyonenwa na nabii Yoeli, “‘Na itakuwa siku za mwisho,” asema Mungu, “Nitamwagia watu wote Roho Yangu. Nitawamwagia watumishi wangu wanawake na watumishi wa kike Roho Yangu, nao watatabiri. Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu na katika nchi chini, na moto, na mvuke, na nguzo ya moshi. Itakuwa, kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na kuogofya, itakuwa kwamba kila atakayeliita Jina la Bwana ataokoka.”’”

232 Ilikuwa kazi la Mungu. Ilikuwa Roho Mtakatifu bali hawakulielewa. Hawakumfahamu vizuri.

233 Yeye kila wakati amekosa kufahamika. Israeli ilikosa kumfahamu. Wale watu katika siku za Nuhu hawakumfahamu. Watu katika siku za Danieli hawakumfahamu. Watu katika siku za Yohana hawakumfahamu vizuri. Watu katika—katika siku za nabii hawakumfahamu. Watu katika siku za Pentekoste hawakumfahamu.

234 Watu siku hizi hawamfahamu, ingali vivyo hivyo. Hawaelewi, kwa sababu Yeye hukosa kufahamika. Ni wakati wa kulinganisha ya kawaida na ya kiroho.

235 Wakati watu katika . . . Na baada ya siku ya Pentekste, wote walipojazwa na Roho Mtakatifu, walikuwa na huu mkutano mkuu kule juu, walikomwita mtu fulani kule chini aliyekuwa

kilema toka tumboni mwa mama yake, wawili wao walikuwa wakitembea barabarani kisha huyu mwombaji akatikisa mkebe na kuomba pesa. Naye alisema, "Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho." Yeye alisema, "Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende!" Naye akamshika huyu mtu mkono na kumwinua juu, mara nyayo zake na vifundo vya miguu yake vikatiwa nguvu. Akaanza kwenda, akirukaruka, na kukimbia na kurukaruka, na kumsifu Mungu, akaingia hekaluni. Na watu wote wakaanza kukusanyika, na kupaza sauti na kuendelea. Naam, lilikuwa lisilo la kawaida.

236 Nao wakawatupa gerezani, na kuwatisha wao kuwa "Wasihubiri tena katika Jina la Yesu.

237 Naye Petro akasema, "Tumsikize nani, Mungu au mwanadamu?"

238 Nao wakawaachilia, wakidhani kwa sababu walikuwa wamewapiga mijeledi kidogo na kuwatisha (kuwa wao wangewanyonga wakati mwingine, au kuwateketeza, au kuwasulubisha msalabani, au cho chote kile), wangeikomesha. Lakini muda si muda, walikuwa barabarani wakifanya hivyo tena. Kwa nini? Hawakufahamu. Haikuwa watu hao; ilikuwa Mungu katika watu hao, akifanya mambo hayo.

239 Walipomkamata maskini Stefano kwenye Baraza kuu la Kiyahudi, asubuhi hiyo, kasema, "Tutampeleka mbele ya mahakama haya. Wakati hawa marabi wote na Wayahudi na makuhani wakuu na baba watakatifu, na wengine wote walipokusanyika pale, hawa wenye shahada za kitheologia litamtisha yeye sana." Kwa hivyo wao walimleta nje katika hizi pingu, na kumsimamisha nje pale, maskini mtu mdogo kama mwana-kondoo kati ya kundi la mbwa mwitu wakali. Wao walisema, "Mtazame akighairi sasa, aseme, 'Nitaghairi, ndugu, msiniudhi.'"

240 Yeye alisema, "Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa mioyo wala maskio! Mbona mnampinga Roho Mtakatifu? Kama vile baba zenu walivyofanya, nanyi ni vivyo hivyo!" Amina!

241 Walitambua haikuwa yeye! Maana walichukua mabonge, wakaziba masikio yao, na kuanza kumsagia meno, na kumpiga hata akafa. Naye alipoinua kichwa chake kuelekea kule, wakimpiga kutoka upande mmoja wa kichwa hadi ule mwingine, yeye alisema, "Naona mbingu zimefunguka, na Yesu ameketi mkono wa kuume wa Mungu." Amina! Naye akalala mikononi mwa Bwana Yesu. Yeye alipokufa, alisema, "Baba, usiwahesabie dhambi hii."

242 Mnaona, hawakufahamu yale aliyofanya. Paulo, akisimama pale akiyatazama, baadaye yalimtatiza, naye akasema, "Mimi ni mdogo kati yao wote, kwa sababu nilishuhudia kifo cha Stefano, mtakatifu Wako." Amina. Ndiyo hiyo.

243 Mnaona, watu hawakufahamu hii shauku. Watu hukosa kufahamu siku hizi. Hukosa kufahamu nguvu za Roho Mtakatifu. Wanaziita kundi la watakatifu wafingirikao. Wanaziita kundi la watu ambao hawana akili timamu. Wanakosa kufahamu. Iliwapasa wapoteze kile wanachokiita "akili zako timamu," ili wa mjue Kristo, kwa sababu una nia ya Kristo ndani yako. Hauwezi kuwa na nia za ulimwengu huu na nia ya Kristo wakati mmoja, moja ni ya kimwili na nyingine ni ya kiroho. "Yeye aenendaye kwa kufuata mambo ya mwili ni wa kimwili, yeye aenendaye kwa kufauta mambo ya kiroho ni wa kiroho." Amina. Kwa hivyo nitajipoteza mwenyewe na kujipata, Bwana, katika Wewe. Naam, bwana. Kwa hivyo Mungu hafahamiki. Si ninyi ambao mmekosa kufahamika, ni Roho Mtakatifu anayewafanya ninyi mfanye hayo ili wao wasifahamu. Amina. Hawaneni dhidi yenu, wananena dhidi Yake. Watu wanakosa kufahamika.

244 Pale, wanaweza kuwaachilia waende, lakini wanarudi moja kwa moja barabarani na kuanza tena. Vivyo hivyo leo. Hawawafahamu hao watu. Hawajui ni nini.

245 Siku hizi mimi sifahamiki katika huduma yangu, kwamba Yeye alinituma kwa watu. Wanakosa kufahamu. Kila mmoja wao alisema, "Tunamwamini Ndugu Branham. . . " Niliongea na mhubiri mmoja muda mchache uliopita, kasema, "Ndugu Branham, sote tunajua ulitumwa kwa Kanisa, lakini, wazo ni kwamba, umekujaje wewe ukibatiza kwa Jina la Yesu?" Wao hawafahamu Maandiko. Wao hawayafahamu. Hilo ndilo Yeye alilonitumia, hilo ndilo kusudi langu la kuwa hapa. "Mbona unafundisha ule uzao wa nyoka, na mambo kama hayo yasiyoambatana na yale tunayofundisha?" Vema, ndugu, hiyo ndiyo sababu niko hapa. Hawafahamu. Amina. Lakini Mungu anatoa ushuhuda kwa Neno Lake na ishara za Roho Mtakatifu katika. . . ?. . . Haidhuru wanavyokosa kufahamu, Mungu anathibitisha Neno! Amina.

246 Mungu kila mara amekosa kufahamika. Na wale wanaoishi pamoja na Mungu wanafahamika vibaya pamoja na Mungu, kwa sababu ni Mungu akifanya kazi ndani yao. Amina. Je, mnaamini?

Nampenda, Nampenda,
Kwani alinipenda kwanza (Je, mwampenda?
  Inueni mikono yenu mkaseme asifiwe). . .
  kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

247 Mna furaha mmekosa kufahamika? Tulizoea kuimba wimbo mdogo, tukisema, *"Sasa, nimetiwa alama, nimetiwa alama, nimetiwa alama, nimetiwa alama na Roho wa Mungu."* Hiyo ni kweli. Watu walionipenda wakati mmoja, wamenipa kisogo sasa kwa sababu nimetiwa alama, nimetiwa alama na Roho. Amina.

Nilipoteza akili zangu kwa vitu vya ulimwengu, nikapokee nia ya Kristo; kwa hivyo, ikiwa nina nia ya Kristo, nia yangu yatafuta vitu vile vilivyo juu. Ningetaka mtu mmoja anionyeshe ubatizo mwingine wo wote ulio sahihi ila katika Jina la Yesu Kristo. Ningetaka mtu mmoja anionyeshe Andiko linalosema nyoka hakuwa na uzao. Ningetaka mtu fulani anionyeshi Andiko linalosema kuna Miungu mitatu.

248 Ndipo wao husema, "Vema, iko wapi?"

249 Mungu alitumia mimi Ujumbe Wake na unaushuhudia. Yeye anathibitisha Neno kwa ishara na maajabu. Hivyo ndivyo Biblia ilisema. Hawawezi kukana hayo, ni kweli. Lakini walifanyaje? Wanakosa kuufahamu kwa sababu sikuja kwa jina la Assemblies of God, Umoja, au Uwili, au Utatu, au Church of God, au Batisti, Methodisti, Presbiteria, Walutheri. Sikuja kwa majina yo yote, naja katika Jina la Yesu Kristo. Na Mungu, kwa neema Zake, na anathibitisha Ujumbe kwa nguvu za kufufuka Kwake Yesu Kristo. Kwa hivyo bado ni Roho wa Mungu ambaye watu wanamfahamu makosa. Hiyo ni kweli, hafahamiki.

250 Hakika, hamfahamiki, wote wanaoishi maisha ya utaua katika Yesu Kristo hawafahamiki. Kote tangu Nuhu mwenye haki, kote kote hata watakatifu wa siku hizi leo, hawafahamiki. Kila mara imekuwa vile, watu hawafahamu.

251 Israeli haikufahamu. Hawafahamu; hawawezi kwa sababu wao ni wa kimwili rohoni, na sio . . . haitatengana na ya kiroho, kwa sababu hayatachanganyikana.

252 Lakini nina furaha kuwa tunaishi katika Ufalme ambao haujatengenezwa kwa mikono ya mwanadamu. Nina furaha kuwa tunaelekea kwenye Ufalme ambao hauhusiani ni mwanadamu. Nina furaha kwamba Ufalme wetu uko juu. Na kama ufalme wetu uko juu, tumezaliwa toka juu, ndipo tunatafuta vitu vile vitokavyo juu, Kristo aketipo mkono wa kuume wa Mungu, lo, ambapo Yeye hatatuonea haya. Ni ushuhuda wetu . . . Hatutamwonea haya duniani humu, kwa sababu sisi ni wasafiri na wageni. Sisi si wa dunia hii, sisi tumezaliwa na Roho wa Mungu. Sisi tunaketi pamoja katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, tumeoshwa katika Damu Yake, tumezaliwa na Roho Wake, tumejazwa na neema Yake.

253 Ndiyo hiyo, hatufahamiki. Lakini, tunajali nini, tunampenda. Je, si mnampenda? Sawa, Teddy, tupe sauti ya *Nampenda,* na hebu tuuimbe toka kilindi cha mioyo yetu:

> Nampenda, Nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

254 Si Yeye ni wa ajabu? Je, si mnampenda? Je, si mna furaha kuwa mu wa kipekee? Ukuhani wa kifalme, watu

waliochaguliwa, watu wa kipekee, tunaotoa dhabihu za roho, matunda ya vinywa vyetu, tukimpa Yeye sifa.

255 Nitaimba wimbo sasa, najisikia kuimba:

Napata watu wengi wasioweza kufahamu
Kwa nini nina furaha tele niko huru;
Nimejazwa na Roho, hamna shaka,
Basi, hiyo ndiyo hoja yangu.

Lo, hiyo ndiyo hoja yangu,
Lo, hiyo ndiyo hoja yangu;
Nimejazwa na Roho, hamna shaka,
Na hiyo ndiyo hoja yangu.

256 Je mwaupenda huo? Hebu tuuimbe basi:

Twapata watu wengu wasioweza kufahamu
Kwa nini tuna furaha tele na sisi ni huru;
Tumejazwa na Roho, hamna shaka,
Na hiyo ndiyo hoja yangu.

Lo, hiyo ndiyo hoja yangu, (Mungu asifiwe!)
Lo, Hiyo ndiyo hoja yangu.
Nimejazwa na Roho, hamna shaka,
Lo, ninapofurahi, ninaimba na kupaza sauti, wengine hawaifahamu, naona;
Lakini nimevuka Yordani nikiingia nchi nzuri ya Kanani,
Basi, hiyo ndiyo hoja yangu.

Lo, hiyo ndiyo hoja yangu, (Mungu asifiwe!)
Lo, hiyo ndiyo hoja yangu;
Nimevuka Yordani nikaingia nchi nzuri ya Kanani,
Basi, hiyo ndiyo hoja yangu.

257 Lo, naupenda huo. Nanyi je? Nimevuka Yordani nikaingia nchi nzuri ya Kanani, nikauaga ulimwengu, nimeinuliwa juu ya vitu vya ulimwengu, sasa ninaishi katika hali hii ya Kimbinguni. Bila shaka naonekana wa kipekee kwa wale nderi kule chini, naam, hakika, naruka juu yake. Hiyo ni kweli. Tunajali nini? Tunaishi katika nchi nzuri ya Kanani. Amina! Naam, bwana. Tunakula Zabibu mpya, huku tukiwa na wakati wa ajabu; uliojaa utukufu, umejawa na nguvu, umejawa na Roho Mtakatifu. Naam, bwana.

258 Ilisemwa kuhusu Stefano, “Alikuwa mtu, aliyejaa.” Aliyejaa nini? Aliyejaa nini? Yeye alijaa Roho Mtakatifu, yeye alijaa nguvu, yeye alijaa hekima, yeye alijaa uweza. Yote yangekuwa nini? Yeye alijaa Roho Mtakatifu! Hapo ndipo vitu hivi vyote hukaa. Hivyo ndivyo kanisa la Mungu aishiye lilivyo. Je, si una furaha, kwa ajili yake Mkiristo? Tenda kwa furaha. Ikiwa hufahamiki, “Wote wanaoishi maisha ya utaua katika Kristo

Yesu watakosa kufahamika.” Kila mara imekuwa vile, kote Bibliani.

259 Sasa, najaribu kusema nini? Kwenu watu mnaonena kwa lugha, kwenu mnaopiga kelele, na kucheza katika Roho, watu husema, “Lo, ni upuzi,” kumbuka tu nimerudi nyuma na kuwaonyesha ninyi. Kote katika Maandiko, wao kila mara wamekosa kufahamika. Kumbuka, wewe uko katika Maandiko, na unatenda yale yaliyo sahihi. Dumu nayo, Mungu yu pamoja nawe. Dumu katika Maandiko, Mungu atashughulikia yaliyobakia. Amina.

260 Nampenda. Hebu tuuimbe wimbo wetu mzuri wa kale wa ubatizo, ule tuliokuwa tukiimba mara ya kwanza Malaika wa Bwana alipotokea mbele ya watu, uweponi mwake. Nilikuwa nimemwona awali, mimi binafsi, lakini wakati wa kwanza Yeye alipowahi kushuka. Naye aliposhuka, ali—alisema, “Kama Yohana alivyotumwa kutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utatangulia kule Kuja kwa Pili kwa Kristo.” Mamia na mamia na mamia ya watu wakisimama kwenye kingo zile kule chini Yeye aliposhuka mwezi wa Juni, 1933, mtoni. Nasi tulikuwa tumesimama kingoni, tukiimba:

Ukingoni mwa Yordani
Ninaangalia
Bara nzuri ya Kanani
Ninayotamani.

Tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata Milele.

Lo, tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata Milele.

Tutapafikia lini,
Na kubarikiwa!
Penye Ufalme wa Baba
Na kumwona uso?

Lo, tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha;
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata Milele.

Bara lile lina Nuru,
Mchana wa Milele,
Kristo juu hutawala,
Hufukuza giza.

Ee, tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata Milele.

261 Hebu tuuimbe tena, na kusalimiana kwa mikono na mtu fulani aliye karibu nawe.

Tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha;
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata Milele.

262 Sasa, bila shaka kamwe, kila mmoja wenu ambaye amemkubali Kristo, na anajua kuwa amezaliwa mara ya pili na Roho, hebu tuinue mikono yetu sasa na kuimba:

Tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata Milele.

263 Sijaona hili kwa muda mrefu. Mabibi, twaeni vibeti vyenu mkachukue vitambaa. Mabwana, tieni mikono yenu mifukoni mwenu na mkatwae vitambaa vyenu. Sasa tutafanya toleo la kumpeperushia Bwana. Vema, sisi sote pamoja, tutapeperusha kama tunaoenda Kanani sasa, peperusheni vitambaa vyenu. Vema sasa:

Tutakaa pamoja na Yesu
Katika Pwani yenye raha
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo
Milele hata Milele.

264 Sasa, kama kuna ye yote hapa ambaye hawajahakikisha uteule na kuitwa kwao, ambao wangependa kuja tunapoimba tena, ningependa mtoe vitambaa vyenu na mkavipeperusha nasi tena. Mlangu umefunguliwa sasa, tikiti ni bure. Mbona usije? Ingia ile meli ya kale ya Sayuni, inaenda, inaondoka. Hebu tuende.

Tutakaa pamoja na Yesu (haitachukua muda mrefu)
Lo, katika Pwani yenye raha;
Tutaimba wimbo wa Musa na Kondoo;
Milele hata Milele.

265 Tunapoinamisha vichwa vyetu:

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
Duniani nataka niwe kama Yeye;
Kote safarini maishani toka duniani hata Utukufuni,
Naomba tu niwe kama Yeye.

Toka hori la Belhelehemu kulitokea mgeni,
Kote safarini Maishani toka duniani hata Utukufuni
Duniani nataka niwe kama Yeye naomba tu niwe kama Yeye.

266 Msisahau Jumapili. Msisahau Jumatano usiku ni mkutano wa maombi. Kumbukeni, ombeni zaidi, niombeeni, ombeeni mchungaji wenu, ombea jirani yako, mashemasi wako, wadhamini wako, omba kuwa Mungu atafanya mapemzi Yake kwetu sote.

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu.
Duniani nataka (Hiyo ndiyo shauku ya Moyo wangu)
Niwe kama Yeye; (Yeye anafahamu) (Ijapokuwa watu wengi hawafahamu, kumbuka kuwa Mungu atatengeneza njia). . .toka duniani hata Utukufuni
Naomba tu niwe kama Yeye.

(Ndugu Branham aanza kuvumisha wimbo huu—Mh.). . .mnyenyekevu na mpole,
Duniani nataka niwe kama Yeye;
Kote safarini ya maishani toka duniani hadi Utukufuni
Naomba tu niwe kama Yeye.

267 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, na macho yetu yamefungwa, na mioyo yetu imeelekezewa Mungu. Tutamwita rafiki yangu Mpendwa, mzuri, Ndugu Roy Borders, toka California, kama yeye. . .ataomba baraka juu ya mkutano huu. Ndugu Borders. [Ndugu Borders aomba—Mh.]

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org